Haliuzwi
JUNI 9, 2026
/islamicftz
Dhul-Hijja 23 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 587
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Samia, Putin waupa nguvu mpya mradi wa madini wa dola bilioni 1.2



# Hisa 15 pekee Afrika Mashariki zakidhi Sharia

- Utafiti mpya umebaini kuwa kampuni 15 pekee kati ya 90 zilizoorodheshwa katika masoko ya hisa ya Tanzania, Kenya na Uganda zinakidhi viwango vya uwekezaji wa Kiislamu
- Kenya yaongoza kwa kampuni nane, huku benki na kampuni za pombe zikiondolewa kwa kukiuka misingi ya Sharia.

## Erdogan: Fedha za Kiislamu mfumo wa uchumi wenye haki zaidi duniani



## Morogoro wapelekewa huduma za matibabu ya macho buree



## Mabalozi wa nchi za Kiarabu wavutiwa na kasi ya Mwinyi maendeleo Zanzibar

- Kwa niaba yao, Balozi wa Saudi Arabia, Yahya Ahmed Okesh, ampongeza Dkt. Mwinyi kwa uongozi wake unaoendelea kuleta mafanikio katika sekta za miundombinu, uchumi na utalii.



Balozi wa Saudi Arabia, Yahya Ahmed Okesh

## Vijanawaaswa kuijenga ndoa kwa mapenzi, subira na uchumi

## Ripoti yadai ongezeko la mauaji ya raia Gaza

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU



# Vijana waaswa kuijenga ndoa kwa mapenzi, subira na uchumi

**Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, alisema Serikali imepokea kwa mikono miwili jitihada zinazofanywa na Al Hikma Foundation katika kuwasaidia vijana kuingia katika ndoa halali na zenye misingi ya maadili**

Katika tukio lililoelezwa kuwa hatua muhimu ya kuimarisha maadili ya Kiislamu na ustawi wa jamii, vijana 130 wamefungishwa ndoa kwa pamoja baada ya kufadhiliwa mahari na Taasisi ya Al Hikma Foundation, huku Serikali ikiahidi kuwafungulia fursa za kiuchumi ili waweze kuhimili majukumu ya kifamilia.

Ndoa hizo za pamoja zilifungwa katika Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, zikihusisha vijana kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya jiji hilo. Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi wa Serikali, viongozi wa dini na mamia ya waumini walioshuhudia tukio hilo lililopewa uzito wa kipekee katika jamii ya Kiislamu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, alisema Serikali imepokea kwa mikono miwili jitihada zinazofanywa na Al Hikma Foundation katika kuwasaidia vijana kuingia katika ndoa halali na zenye misingi ya maadili.

Katambi alisema Serikali itashirikiana na taasisi hiyo kwa kuiunganisha na mamlaka mbalimbali zinazotoa mikopo, mafunzo, ajira na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ili kuhakikisha vijana hao wanapata uwezo wa kujitegemea na kutunza familia zao.

"Tutatumia fursa hii kuwaunganisha vijana hawa na taasisi za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ili waweze kunufaika na mikopo, ajira na programu mbalimbali za maendeleo. Tunataka ndoa hizi ziwe mwanzo wa maisha bora na si chanzo cha changamoto za kiuchumi," alisema.

Aidha, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Temeke pamoja na viongozi wa halmashauri kuhakikisha vijana hao wanapatiwa kipaumbele katika mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Katambi alisisitiza kuwa familia ndiyo msingi wa amani na maendeleo ya taifa, akieleza kuwa kuvunjika kwa maadili ndani ya familia kunaweza kuzalisha kizazi kisichozingatia sheria na maadili ya jamii.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Al Hikma Foundation, Sheikh Nurdin Kishki, alisema vijana hao walipatikana baada ya mchakato maalumu ulioanza Machi 1 mwaka huu wakati wa mashindano ya kimataifa ya Qur'an ambapo taasisi hiyo ilitangaza mpango wa kusaidia vijana wenye nia ya kuoa.

Alisema miongoni mwa masharti yaliyowekwa ni pamoja na mwanamke kuchukua fomu kwa niaba ya mtarajiwa wake, wazazi wa pande zote kuridhia ndoa, na kijana kuwa na shughuli ya kumuingizia kipato. Alieleza kuwa vigezo hivyo vililenga kuhakikisha ndoa zinazofungwa zinakuwa na msingi imara wa kudumu.

"Tumegundua kuwa changamoto kubwa katika ndoa nyingi ni ukosefu wa maandalizi ya maisha ya familia. Ndiyo maana kabla ya kufungishwa ndoa vijana hawa walipatiwa mafunzo ya ndoa, malezi na uwajibikaji," alisema Sheikh Kishki.

Kwa mujibu wa Al Hikma Foundation, hadi sasa zaidi ya vijana 500 wamefadhiliwa mahari na taasisi hiyo, hatua inayotajwa kuwa miongoni mwa juhudi kubwa za kijamii zinazolenga kuwasaidia vijana kuanzisha familia kwa mujibu wa mafundisho ya dini ya Kiislamu.

NA MWANDISHI WETU

# Hisa 15 Kenya, Uganda, Tanzania zatajwa kukidhi Sharia

Utafiti mpya wa hisa zinazokidhi misingi ya Sharia katika Afrika Mashariki umebaini kuwa ni kampuni 15 pekee kati ya 90 zilizoorodheshwa katika masoko ya hisa ya Tanzania, Kenya na Uganda ambazo zinakidhi vigezo vya uwekezaji wa Kiislamu kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya AAOIFI.

Ripoti ya Mei 2026 iliyotolewa na Siraat Shariah Audit and Advisory ilichunguza kampuni zote zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Soko la Hisa la Nairobi (NSE) na Soko la Hisa la Uganda (USE), ikibaini kuwa kampuni 55 ziliondolewa katika hatua ya kwanza ya uchunguzi kutokana na aina ya shughuli zake, huku kampuni 35 zikifikishwa katika hatua ya uchambuzi wa viashiria vya kifedha.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Kenya imeongoza kwa kuwa na kampuni nane zinazokidhi Sharia, ikifuatiwa na Tanzania yenye kampuni tano na Uganda yenye kampuni mbili. Hivyo, kiwango cha jumla cha kampuni zilizofaulu ni asilimia 16.7 pekee ya kampuni zote zilizochunguzwa.

Kampuni za Tanzania zilizotajwa kuwa zinakidhi vigezo hivyo ni Tanzania Portland Cement (TPCC), Tanga Cement Company (TCC), Vodacom Tanzania, Swissport Tanzania na TOL Gases.

Nchini Kenya, kampuni zilizofaulu ni pamoja na Safaricom, Bamburi Cement, Sasini PLC na Williamson Tea Kenya, huku Uganda ikiwakilishwa na Cipla Quality Chemical Industries na Airtel Uganda.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa kampuni nyingi zilishindwa kutokana na kujihusisha na benki za kawaida, bima za kawaida, pombe au tumbaku, ambazo haziruhusiwi chini ya misingi ya Sharia.

Miongoni mwa kampuni zilizotajwa kushindwa uchunguzi huo ni CRDB Bank, NMB Bank, KCB Group, Stanbic Bank Uganda, Tanzania Breweries na East African Breweries.

Aidha, MTN Uganda imewekwa kwenye orodha ya uangalizi baada ya kukosa sifa kwa tofauti ndogo ya asilimia 0.11 juu ya kiwango kinachoruhusiwa cha mapato yasiyokubalika chini ya Sharia.

Waandaaji wa ripoti hiyo wanasema matokeo hayo yanaonyesha kuwa uwekezaji unaozingatia Sharia unaendelea kupata nafasi katika Afrika Mashariki na unaweza kuwa chaguo kwa wawekezaji wanaotafuta uwekezaji wa maadili, uwazi na shughuli zinazohusiana moja kwa moja na uchumi halisi.

Uchunguzi huo ulizingatia vigezo viwili vikuu. Kwanza, aina ya biashara ya kampuni husika, ambapo kampuni zinazojihusisha na riba, bima za kawaida, pombe, tumbaku, kamari na shughuli nyingine zisizoruhusiwa chini ya Sharia ziliondolewa moja kwa moja.

Pili, viashiria vya kifedha vilivyohusisha kiwango cha madeni yanayotegemea riba, mapato yatokanayo na shughuli zisizokubalika na uwiano wa mali za kampuni, kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya Shirika la Uhasibu na Ukaguzi kwa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI).

Hata hivyo, waandaaji wa ripoti hiyo , Siraat Shariah Audit and Advisory, wametanabaisha kuwa itumike kwa ajili ya elimu na taarifa pekee, na yaliyomo si ushauri wa uwekezaji, mwaliko wa kununua au kuuza hisa, wala fatwa ya kidini.

# Wadau wasifu waqfu wa fedha wa PBZ Ikhlas kufadhili elimu

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kupitia dirisha lake la huduma za kifedha za Kiislamu, PBZ Ikhlas, imeanzisha mpango wa Cash Waqf kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa fedha za kufadhili wanafunzi wa elimu ya juu nchini, mpango ambao umepongezwa na wadau.

Katika mpango huo, PBZ itashirikiana na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ambayo itahusika katika kusimamia matumizi ya fedha hizo.

Meneja wa Uzingatiaji wa Sharia wa PBZ IKHLAS, Dkt. Issa Salim Mohamed, amesema katika mahojiano na gazeti la IMAAN kuwa mpango huo unatoa fursa kwa watu binafsi, taasisi, wafanyabiashara, wahisani na wawekezaji kuchangia fedha taslimu kama waqfu ili kusaidia vijana wenye uwezo wa kitaaluma lakini wanaokabiliwa na changamoto za kifedha kuendelea na masomo.

Dkt. Issa alieleza kuwa fedha zitakazotolewa zitawekwa katika akaunti maalumu ya waqfu na kuwekezwa kwa kuzingatia misingi ya Sharia. Faida itakayopatikana kutokana na uwekezaji huo ndiyo itakayowasilishwa kwa HESLB kwa ajili ya kusaidia wanafunzi watakaokidhi vigezo vya kupata ufadhili.

"Lengo ni kujenga mfuko endelevu utakaosaidia vijana wengi zaidi kupata elimu ya juu bila kutegemea michango ya mara moja," alisema.

Makubaliano ya ushirikiano kati ya PBZ na HESLB yalisainiwa jijini Tanga katika hafla iliyohudhuriwa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (Mb), sambamba na uzinduzi rasmi wa tawi la PBZ IKHLAS katika jiji hilo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alisema ushirikiano huo unalenga kupanua vyanzo vya rasilimali fedha ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo na ufadhili wa elimu ya juu.

Alisema mpango huo utasaidia hasa vijana wanaojiunga na vyuo vya kati na mafunzo ya amali, ambao baada ya kuhitimu watachangia maendeleo ya viwanda na sekta nyingine za uzalishaji nchini.

NA MWANDISHI WETU



# Mabalozi wa Kiarabu wampongeza Mwinyi kwa kasi ya maendeleo Z'bar

**Kwa niaba yao, Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania, Yahya Ahmed Okesh, alimpongeza Dkt. Mwinyi kwa uongozi wake unaoendelea kuleta mafanikio katika sekta za miundombinu, uchumi na utalii.**

Zanzibar. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nchi za Kiarabu kuja kuwekeza Zanzibar, akieleza kuwa visiwa hivyo vina mazingira mazuri ya biashara na fursa nyingi zinazoweza kuimarisha uchumi wa pande zote.

Rais Dkt. Mwinyi alitoa kauli hiyo leo, Ikulu Zanzibar, alipokutana na mabalozi wa nchi mbalimbali za Kiarabu wanaoziwakilisha nchi zao nchini Tanzania. Mabalozi hao walifika kwa lengo la kumpongeza kwa mafanikio ya maendeleo yanayopatikana Zanzibar chini ya uongozi wake.

Katika mazungumzo hayo, Dkt. Mwinyi alisema Zanzibar imeendelea kufanya mageuzi mbalimbali ya kiuchumi na kisheria yaliyolenga kuboresha mazingira ya uwekezaji, jambo ambalo limeongeza imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Alitaja sekta za utalii, uchumi wa buluu, mafuta na gesi, uvuvi, utalii wa mikutano na maendeleo ya Bandari Jumuishi ya Mangapwani kuwa miongoni mwa maeneo yenye fursa kubwa kwa wawekezaji kutoka mataifa ya Kiarabu.

"Zanzibar iko tayari kupokea wawekezaji zaidi kutoka nchi za Kiarabu. Tunathamini mchango wao katika maendeleo yetu na tunaamini ushirikiano huu unaweza kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wetu na mataifa yetu," alisema Dkt. Mwinyi.

Rais huyo pia alizishukuru nchi hizo kwa kuendelea kuimarisha ushirikiano na Zanzibar kupitia misaada na uwekezaji katika sekta za elimu, afya na miundombinu. Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuongeza ushirikiano katika teknolojia ya kidijitali, ubunifu na utoaji wa mafunzo kwa vijana ili kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kisasa.

Kwa upande wao, mabalozi hao walieleza kuridhishwa na hatua za maendeleo zinazoshuhudiwa Zanzibar katika miaka ya karibuni. Kwa niaba yao, Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania, Yahya Ahmed Okesh, alimpongeza Dkt. Mwinyi kwa uongozi wake unaoendelea kuleta mafanikio katika sekta za miundombinu, uchumi na utalii.

Alisema maendeleo hayo yanaifanya Zanzibar kuendelea kujijengea sifa kama moja ya vituo muhimu vya uwekezaji, biashara na utalii katika ukanda wa Afrika Mashariki, huku akiahidi kuwa nchi za Kiarabu zitaendelea kuimarisha ushirikiano na kuangalia fursa mpya za uwekezaji katika visiwa hivyo.

ذو الحجة




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na Ikulu, Zanzibar

0629 999 998

## Rais Mwinyi alitoa kauli hiyo leo, Ikulu Zanzibar, alipokutana na mabalozi wa nchi mbalimbali za Kiarabu wanaoziwakilisha nchi zao nchini Tanzania













NA MWANDISHI WETU

# Morogoro wapelekewa huduma za matibabu ya macho bure



Wananchi wa Morogoro na maeneo ya jirani wanatarajiwa kunufaika na huduma za bure za uchunguzi na matibabu ya macho kupitia kambi maalumu itakayofanyika kuanzia Juni 15 hadi 18 mwaka huu.

Kambi hiyo imeandaliwa na Taasisi ya The Islamic Foundation kwa ufadhili wa Mercy Outreach Global na itafanyika katika Kituo cha Al-Jamih for Mother and Child Health Care kilichopo Msamvu, karibu na Ofisi za Uhamiaji.

Mkurugenzi wa Utawala wa The Islamic Foundation, Arafat Badru, amesema huduma hizo zitatolewa na madaktari bingwa wa macho kutoka Wizara ya Afya, ambao watafanya uchunguzi wa kina kwa wagonjwa wote watakaofika.

Badru amesema matibabu yatakayopatikana ni pamoja na upasuaji wa mtoto wa jicho, utoaji wa miwani na dawa kulingana na mahitaji ya mgonjwa.

Inakadiriwa kuwa takribani wagonjwa 250 watapatiwa upasuaji wa mtoto wa jicho bila malipo wakati wa kambi hiyo.

Amehimiza wananchi wenye matatizo ya macho kutumia fursa hiyo mapema ili kupata uchunguzi na matibabu stahiki.

Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma hizo, wananchi wametakiwa kuwasiliana kupitia namba 0747 338 799.

# Wapenda kheri waaswa kujiandikisha uchangiaji kila mwezi Imaan Media

Waislamu na Watanzania kwa ujumla wanaounga mkono kazi za Vyombo vya Habari vya Imaan wamehimizwa kujiandikisha katika mpango wa kadi za wachangiaji ili kuchangia kwa utaratibu maendeleo na uendelevu wa vyombo hivyo.

Taasisi ya The Islamic Foundation, inayomiliki vyombo vya habari vya Imaan, imesema usajili unaendelea kwa watu binafsi, familia, wafanyabiashara na taasisi zinazotaka kuwa sehemu ya juhudi za kuendeleza da'awah, elimu na habari zenye maadili ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa taasisi hiyo, mpango huo unalenga kujenga mfumo endelevu wa michango ya kila mwezi utakaoziwezesha Radio Imaan, TV Imaan na Gazeti Imaan na majukwaa mengine ya taasisi kuendelea kutoa huduma kwa jamii na kupanua wigo wa kufikia wasikilizaji na wasomaji wengi zaidi.

Awali, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Nahdi, alisema sehemu ya fedha zitakazopatikana kupitia mpango huo zitatumika katika juhudi za kuipanua Radio Imaan ili kufikisha matangazo yake katika mikoa mingi zaidi nchini.

Mpango huo una makundi mbalimbali ya kadi kulingana na kiwango cha mchango wa kila mwezi. Makundi hayo ni Platinum (Sh500,000), Gold (Sh300,000), Silver (Sh200,000), Bronze (Sh100,000), Green (Sh10,000), Blue (Sh5,000) na Maroon (Sh1,000).

Wananchi wanaotaka kujiunga na mpango huo wametakiwa kutuma majina yao matatu, wilaya na mkoa wanaoishi pamoja na aina ya kadi wanayoihitaji kupitia namba 0671 444 555.

Pia wanaweza kujaza fomu ya usajili kupitia kiungo: https://forms.gle/XHpkojc7vkW-cA3d17

Taasisi hiyo imeeleza kuwa baada ya usajili kukamilika na kadi kuandaliwa, mwombaji ataarifiwa namna ya kuipokea. Wadau wamehimizwa kutumia fursa hiyo kuwa sehemu ya kuimarisha vyombo vya habari vya Kiislamu na kusaidia kuendeleza kazi ya da'awah nchini.

NA MWANDISHI WETU
DODOMA

# Samia afungua ukurasa mpya wa ushirikiano wa madini na Russia, mradi wa dola bilioni 1.2 wapata nguvu mpya

Mradi mkubwa wa uchimbaji wa urani wa Mkuju River uliopo Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma umepewa msukumo mpya kufuatia ziara rasmi ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Russia, huku Serikali ikieleza kuwa uwekezaji huo wa kimkakati sasa unaelekea katika hatua za utekelezaji kamili baada ya miaka mingi ya kusuasua.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, amesema mazungumzo yaliyofanyika kati ya viongozi wa Tanzania na Russia yameimarisha dhamira ya pande zote kuhakikisha mradi huo unaanza kuzalisha matokeo yaliyokusudiwa na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa urani barani Afrika.


Akizungumza akiwa Moscow pembeni mwa ziara ya Rais Samia, Mavunde alisema mradi huo unaotekelezwa na Mantra Tanzania Limited, kampuni tanzu ya Uranium One Group chini ya Shirika la Serikali ya Russia la Rosatom, ni miongoni mwa miradi muhimu zaidi ya madini inayotarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mradi huo wenye thamani ya dola bilioni 1.2 za Marekani umeendelea kupata mafanikio makubwa baada ya kukwama kwa zaidi ya muongo mmoja kutokana na kushuka kwa bei ya urani katika soko la dunia pamoja na changamoto za upatikanaji wa fedha za uwekezaji.

"Mkuju River ni mradi wa kimkakati kwa sekta ya madini na uchumi wa taifa kwa ujumla. Tanzania ni miongoni mwa nchi chache Afrika zenye uwezo wa kuendeleza sekta ya urani kwa kiwango hiki kikubwa," alisema Mavunde.

Alibainisha kuwa ziara ya Rais Samia imefungua fursa ya mazungumzo ya moja kwa moja na mamlaka za Russia pamoja na wadau wa mradi huo, jambo ambalo limeongeza matumaini ya kuona hatua kubwa zikifikiwa ndani ya muda mfupi.

Mavunde alitaja uzinduzi wa kiwanda majaribio cha kuchakata urani uliofanywa na Rais Samia mwezi Julai mwaka jana kuwa ushahidi kwamba mradi huo umeingia katika hatua za utekelezaji na umevuka kipindi cha mipango pekee.



Aidha, alisema zabuni za ujenzi wa miundombinu muhimu katika eneo la mradi tayari zimetangazwa na shughuli mbalimbali za awali za uchimbaji zinaendelea kwa mujibu wa sheria na masharti ya leseni ya uchimbaji.

Licha ya kuwepo kwa maswali kuhusu ufadhili wa mradi huo na muda wa leseni ya uchimbaji unaotarajiwa kuisha mwaka 2028, Waziri huyo alisema Serikali ina imani kuwa changamoto hizo zitapatiwa ufumbuzi kupitia mifumo iliyopo kisheria, ikiwemo uwezekano wa kuongeza muda wa leseni hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa za Mantra Tanzania, mazungumzo ya kupata fedha yanaendelea kati ya taasisi za kifedha za Russia na benki za Tanzania ili kuwezesha ujenzi wa mgodi na kiwanda kikubwa cha uchakataji urani.

Mavunde alisema mradi huo ukikamilika unatarajiwa kuzalisha zaidi ya tani 4,000 za urani kwa mwaka na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili mkubwa wa urani barani Afrika baada ya Namibia.

Aliongeza kuwa uwekezaji huo utazalisha maelfu ya ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, kuongeza mapato ya Serikali na kuchochea shughuli za biashara katika Mkoa wa Ruvuma.

ذُو الحِجَّة



NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi: Jukwaa la Uwekezaji laifungua Zanzibar kwa dunia

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema mafanikio ya Jukwaa la Uwekezaji Zanzibar 2026 yamefungua ukurasa mpya wa fursa za uwekezaji, ushirikiano wa kimataifa na ukuaji wa uchumi wa Zanzibar.

Akizungumza katika hafla ya Presidential Gala Dinner iliyofanyika katika Hoteli ya Diamond Bijoux, Bwejuu, Dkt. Mwinyi alisema jukwaa hilo limeiwezesha Zanzibar kujitangaza zaidi katika ramani ya kimataifa kama eneo lenye fursa nyingi za uwekezaji na mazingira rafiki kwa wafanyabiashara.

Alieleza kuwa ushiriki mkubwa wa wawekezaji, viongozi wa biashara na wadau wa maendeleo kutoka mataifa mbalimbali duniani ni ishara ya kuongezeka kwa imani ya jumuiya ya kimataifa katika uchumi wa Zanzibar na mwelekeo wake wa maendeleo.

Rais Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuweka mazingira bora zaidi ya uwekezaji kupitia uwazi, uwajibikaji na utekelezaji wa mageuzi yanayolenga kuongeza ufanisi katika taasisi na sekta zinazohusika na biashara na uwekezaji.

"Tunatambua mchango mkubwa wa sekta binafsi katika kukuza uchumi. Serikali itaendelea kushirikiana na wawekezaji kwa kuhakikisha mazingira ya biashara yanabaki kuwa ya kuvutia na yenye ushindani," alisema.

Aidha, aliipongeza Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa maandalizi na utekelezaji wa jukwaa hilo ambalo limewakutanisha washiriki zaidi ya 600 kutoka sehemu mbalimbali duniani. Alisema mafanikio hayo yanaonesha uwezo wa Zanzibar kuvutia mikutano mikubwa ya kimataifa na kujijengea hadhi kama kitovu cha uwekezaji katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Katika hafla hiyo, Dkt. Mwinyi alitunukiwa Tuzo Maalum ya Uongozi katika Maendeleo ya Sekta ya Uwekezaji Zanzibar iliyotolewa na ZIPA, ikiwa ni kutambua mchango wake katika kuimarisha sera, mifumo na mazingira yanayowezesha ukuaji wa uwekezaji nchini.

Mbali na hafla hiyo, Rais Mwinyi pia alikutana na Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), ambapo aliwahimiza kutumia fursa zilizopo Zanzibar kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi. Alisema diaspora wana mchango mkubwa si tu kwa mtaji wa kifedha, bali pia kwa maarifa, utaalamu na teknolojia wanazoweza kuiletea nchi.

Alisisitiza kuwa ushiriki wa Watanzania waishio nje katika miradi ya maendeleo utasaidia kuongeza ajira, kuimarisha ushindani wa uchumi na kuharakisha safari ya Zanzibar kuelekea uchumi wa kisasa na jumuishi.



KUTOKA KWA MAJIRANI

UKHT FATIMA SS

# Msikiti Mkuu wa nchini Uganda watajwa miongoni mwa vivutio vya utalii wa kidini

***KAMPALA*** — Uganda imehimizwa kuwekeza zaidi katika utalii wa kidini, huku Msikiti Mkuu wa Taifa wa Uganda ukitajwa kuwa miongoni mwa vivutio muhimu vinavyoweza kuvutia maelfu ya wageni kutoka Afrika na sehemu nyingine za dunia.


Katika makala iliyochapishwa na Observer Uganda, mwandishi Alice Nalweera amesema utalii wa kidini ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi duniani na unaweza kusaidia Uganda kuongeza mapato ya fedha za kigeni na ajira.

Makala hiyo imeutaja Msikiti Mkuu wa Uganda uliopo Kampala kuwa moja ya misikiti mikubwa zaidi barani Afrika na alama muhimu ya urithi wa Kiislamu nchini humo. Msikiti huo huvutia Waislamu kutoka nchi mbalimbali za Afrika Mashariki na maeneo mengine duniani.

Nalweera amesema pamoja na vivutio vya Kikristo na vya tamaduni za asili, maeneo ya Kiislamu yana nafasi kubwa ya kuifanya Uganda kuwa kitovu cha utalii wa kidini katika ukanda huo.

Kwa mujibu wa makala hiyo, wageni wa kidini huchangia uchumi kupitia matumizi ya malazi, usafiri, chakula na huduma nyingine, hivyo kusaidia kuongeza ajira na maendeleo ya jamii zinazozunguka maeneo ya ibada.

Mwandishi ameitaka serikali ya Uganda kuboresha miundombinu na kuitangaza zaidi historia na urithi wa dini mbalimbali ili kunufaika na soko la kimataifa la utalii wa kidini.



# Mahujaji wa Kenya wasifu maandalizi ya Hijja 2026

***NAIROBI*** — Mahujaji wa Kenya walioshiriki Hijja ya mwaka 2026 wamepongeza maandalizi na huduma zilizotolewa nchini Saudi Arabia, wakisema ibada ya mwaka huu imekuwa miongoni mwa zilizoandaliwa vizuri zaidi katika miaka ya karibuni

Kwa mujibu wa gazeti la Eastleigh Voice, mahujaji hao walitaja maboresho makubwa katika malazi, usafi wa mazingira, huduma za ustawi na uratibu wa shughuli mbalimbali za Hijja ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Sheikh Muhamad Alwy alisema kila kitu kilikuwa cha utaratibu tangu mwanzo hadi mwisho wa safari hiyo, huku mahujaji wengine wakibainisha kuwa mahema na huduma za makazi ziliboreshwa kwa kiwango kikubwa.

Kassim, ambaye amefanya Hijja mara saba, alisema mwaka huu kulikuwa na maendeleo makubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo kulikuwa na changamoto za malazi.

Hata hivyo, maafisa wa afya waliripoti kuwa mamia ya mahujaji wa Kenya walipata matibabu kutokana na mafua na maradhi mengine yaliyosababishwa na hali ya hewa na vumbi. Mkurugenzi wa Afya na Usafi wa Baraza Kuu la Waislamu Kenya (SUPKEM), Dkt. Hussein Iman, alisema takribani mahujaji 1,350 walihudumiwa na timu za afya wakati wa Hijja.

Katibu wa maandalizi wa SUPKEM, Juma Musa Osman, alisema mafanikio hayo yalitokana na mipango na maandalizi ya kina yaliyofanyika kabla ya safari hiyo.

UKHT FATIMA SS




# Ripoti yadai ongezeko la mauaji ya raia wa Palestina Gaza

Kituo cha Palestina cha Haki za Binadamu (PCHR) kimeripoti ongezeko kubwa la mauaji ya raia wa Palestina katika Ukanda wa Gaza mwezi Mei, kikidai kuwa hali hiyo ni sehemu ya kampeni ya kimfumo dhidi ya Wapalestina.

Kwa mujibu wa taarifa ya kituo hicho, watu 119 waliuawa mwezi Mei pekee, wakiwemo watoto 19 na wanawake 10, huku wanawake, watoto na wazee wakifanya karibu asilimia 30 ya vifo vyote vilivyoripotiwa.

PCHR ilisema mashambulizi ya Israel yalilenga maeneo mbalimbali ya Gaza, yakiwemo Gaza City, Khan Younis, Deir al-Balah na kambi za wakimbizi, ambapo familia kadhaa zilipoteza maisha.

Wakati huo huo, wakili wa daktari wa Kipalestina Hussam Abu Safiya amesema mteja wake, ambaye ni mkurugenzi wa Hospitali ya Kamal Adwan, amehamishiwa katika kifungo cha upweke katika gereza la Nafha nchini Israel na kunyimwa huduma za matibabu za kutosha.

Ripoti hiyo pia ilieleza kuwa operesheni za kijeshi na mashambulizi ya walowezi wa Kiyahudi zimeendelea katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu, ambapo mali na mifugo ya Wapalestina imeripotiwa kushambuliwa. Israel imekuwa ikisisitiza kuwa operesheni zake zinalenga makundi yenye silaha yanayopigana nayo katika Gaza.

## Trump akerwa wabunge kukataa vita, asema hawana uzalendo

**WASHINGTON — Rais wa Marekani Donald Trump amelaani kura ya Baraza la Wawakilishi iliyopitisha azimio la kutaka kuzuia hatua zaidi za kijeshi dhidi ya Iran, akiwaita wabunge walioiunga mkono "wasio na uzalendo" na wanaohatarisha juhudi za kumaliza mgogoro huo.**

**Kupitia mtandao wake wa Truth Social, Trump alisema kura hiyo imefanyika wakati utawala wake ukiwa katika hatua za mwisho za mazungumzo ya kumaliza vita kati ya Marekani na Iran.**

**"Ni nani angefanya jambo lisilo la kizalendo kama hili?" aliandika Trump, akiwashutumu Democrats pamoja na wabunge wanne wa Republican waliopiga kura dhidi ya msimamo wake.**

**Kauli hiyo imekuja siku moja baada ya Baraza la Wawakilishi, wakiwemo wanne wa chama cha Trump, kupitisha azimio la mamlaka ya vita kwa kura 215 dhidi ya 208.**

**Azimio hilo linamtaka Trump kuondoa majeshi ya Marekani katika mapigano dhidi ya Iran au kupata idhini ya Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Vita ya mwaka 1973.**

**Mvutano kati ya Washington na Tehran umeendelea tangu mashambulizi ya Marekani na Israel dhidi ya Iran mwishoni mwa Februari. Ingawa usitishaji wa mapigano ulianza Aprili 8, mashambulizi ya pande zote yameendelea kuripotiwa katika wiki za karibuni.**

## Jaji afuta sera za Donald Trump dhidi ya wahamiaji wa nchi 39

**WASHINGTON — Jaji wa Shirikisho nchini Marekani, John McConnell, amefuta mfululizo wa sera za utawala wa Rais Donald Trump zilizokuwa zimezuia maombi ya hifadhi, vibali vya kazi, ukaazi wa kudumu na uraia kwa wahamiaji kutoka nchi 39.**

**Katika uamuzi wake uliotolewa Ijumaa, McConnell alisema Idara ya Huduma za Uraia na Uhamiaji ya Marekani (USCIS) ilitekeleza sera hizo bila mamlaka ya kisheria na kuwaacha maelfu ya wahamiaji katika hali ya kutokuwa na uhakika wa kisheria kwa miezi mingi.**

**Jaji huyo alisema wahamiaji hao walifuata taratibu zote zilizowekwa na sheria za Marekani lakini maombi yao yalikwamishwa kwa sababu ya nchi walizozaliwa.**

**Sera hizo zilipitishwa baada ya tukio la Novemba mwaka jana ambapo walinzi wawili wa Jeshi la Taifa walishambuliwa mjini Washington, tukio ambalo waendesha mashtaka wanadai lilihusisha mhamiaji kutoka Afghanistan.**

**Baada ya tukio hilo, Trump alitangaza hatua kali za kudhibiti uhamiaji na kupanua marufuku za usafiri kwa nchi 39, zikiwemo Afghanistan, Iran, Haiti, Somalia, Venezuela na Syria.**

**Utawala wa Trump ulikuwa umetetea sera hizo kwa hoja za usalama wa taifa na udhibiti wa uhamiaji.**

## HABARI MASHARIKI YA KATI

UKHTI FATIMA SS



# Masharti mapya ya adhana gumzo kwa Waislamu Al-Aqsa

Hatua ya kamati ya mawaziri wa Israel kuidhinisha muswada unaolenga kudhibiti matumizi ya vipaza sauti misikitini imezua wasiwasi mkubwa miongoni mwa Waislamu na watetezi wa uhuru wa kuabudu.

Muswada huo unapendekeza misikiti kupata kibali maalumu kabla ya kurusha adhana kwa vipaza sauti, huku ukiweka adhabu ya faini inayoweza kufikia shekeli 50,000 (zaidi ya Shilingi Milioni 44 za Kitanzania) kwa ukiukwaji wa masharti hayo.

Hatua hiyo inaweza kuathiri moja kwa moja uhuru wa ibada katika Msikiti wa Al-Aqsa na maeneo mengine matakatifu ya Kiislamu. Takwimu za UNESCO zinaonyesha kuwa Mji wa Kale wa Jerusalem ni eneo lenye urithi wa dunia lenye umuhimu mkubwa kwa mabilioni ya waumini wa dini mbalimbali duniani, huku Al-Aqsa ikiwa miongoni mwa maeneo matakatifu zaidi kwa Waislamu.

Tume ya Kiislamu na Kikristo ya Kuitetea Jerusalem imeonya kuwa vikwazo dhidi ya mamlaka ya Waqf inayosimamia maeneo matakatifu vinaweza kudhoofisha usimamizi wa maeneo hayo. Jordan, ambayo imekuwa mlezi wa kihistoria wa maeneo matakatifu ya Kiislamu na Kikristo Jerusalem tangu mwaka 1924, imeendelea kusisitiza kulindwa kwa hadhi na mfumo uliopo ili kuzuia migogoro mipya katika eneo hilo.

## Zaidi ya visa 190,000 za Umrah zatolewa ndani ya wiki tatu

**RIYADH — Saudi Arabia imetoa zaidi ya visa 190,000 vya Umrah kwa mahujaji kutoka nje ya nchi tangu kuanza kwa msimu mpya wa Umrah mwezi huu, ikiwa ni ishara ya ongezeko kubwa la mahitaji ya ibada hiyo baada ya kumalizika kwa Hijja 2026.**

**Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Hijja na Umrah iliyonukuliwa na Saudi Gazette, visa hivyo vilitolewa kuanzia Dhul Hijjah 14, inayolingana na Juni 10, kupitia jukwaa la kidijitali la Nusuk.**

**Wizara hiyo ilieleza kuwa vibali vya Umrah vilianza kutolewa Juni 11 kupitia programu ya Nusuk, ambayo inawawezesha mahujaji kuhifadhi nafasi, kupata vibali na kufikia huduma mbalimbali za serikali kwa njia ya mtandao.**

**Taarifa hiyo ilisema ongezeko hilo la maombi ya visa limechochewa na mafanikio ya msimu wa Hijja 2026, ambao ulihusisha maboresho katika taratibu, miundombinu ya kiteknolojia na utoaji wa huduma kwa mahujaji.**

**Wizara imeeleza kuwa hatua hizo ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Saudi Arabia 2030 inayolenga kuboresha huduma kwa wageni wa Misikiti Miwili Mitakatifu na kuongeza viwango vya usalama, urahisi na kuridhika kwa mahujaji wanaotembelea Makka na Madina.**

UKHTI FATIMA SS




# Erdogan: Fedha za Kiislamu mfumo wa uchumi wenye haki zaidi duniani



***ISTANBUL***— Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan amesema fedha za Kiislamu zina uwezo wa kuchangia ujenzi wa mfumo wa uchumi wa dunia wenye haki zaidi na unaowajumuisha watu wengi zaidi, wakati dunia ikiendelea kukabiliwa na changamoto za kifedha na kiuchumi.

Akizungumza katika Mkutano wa Tatu wa Uchumi wa Kiislamu Duniani uliofanyika katika Kituo cha Fedha cha Istanbul, Erdogan alisema fedha za Kiislamu ni sehemu muhimu ya urithi wa ustaarabu wa Kiislamu na zina mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi.

Alisema mfumo huo unatoa mbinu ya kifedha inayozingatia maadili, uzalishaji, ushirikiano na haki badala ya kuendeshwa na faida pekee.

"Fedha za Kiislamu si mfumo mbadala kwa Waislamu pekee, bali ni mfano wa haki zaidi na salama kwa ulimwengu mzima," alisema Erdogan.

Rais huyo aliongeza kuwa fedha za ushiriki (participation finance) zinaweza kusaidia kujenga mfumo wa uchumi unaostahimili misukosuko, kuchochea maendeleo ya kweli ya uchumi na kuimarisha uthabiti wa kifedha.

Mkutano huo umewakutanisha viongozi wa serikali, benki kuu, taasisi za fedha, wawekezaji na wataalamu kutoka mataifa mbalimbali kujadili nafasi ya fedha za Kiislamu katika maendeleo endelevu na ustawi wa uchumi wa dunia.

# Uzbekistan yapiga hatua kuelekea benki za Kiislamu

**TASHKENT— Uzbekistan imechukua hatua mpya kuelekea kuanzishwa kwa benki za Kiislamu baada ya Benki Kuu ya nchi hiyo kuwasilisha rasimu ya kanuni zitakazoweka utaratibu wa usajili na utoaji leseni kwa taasisi zitakazotoa huduma za kifedha zinazozingatia Sharia.**

**Kwa mujibu wa Trend News Agency, rasimu hiyo itawezesha kuanzishwa kwa benki mpya za Kiislamu, kufunguliwa kwa "madirisha ya Kiislamu" ndani ya benki za kawaida na hata kubadilishwa kwa benki za kawaida kuwa benki za Kiislamu.**

**Hatua hiyo inakuja wakati huduma za fedha za Kiislamu nchini humo zikionyesha ukuaji mkubwa.**

**Taarifa ya Benki Kuu iliyonukuliwa na UzDaily ilionyesha kuwa taasisi nne za mikopo midogo zilitoa huduma za kifedha za Kiislamu zenye thamani ya soum bilioni 11.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, ongezeko la karibu mara nane ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.**

UKHTI FATIMA SS




# Mapokezi chanja ujio kanuni masoko ya mitaji ya Kiislamu Rwanda

***KIGALI*** — Rwanda ina matumaini kwamba kuanzishwa kwa bidhaa za masoko ya mitaji ya Kiislamu kutafungua chanzo kipya cha fedha kwa ajili ya miradi ya miundombinu, makazi, kilimo na maendeleo ya sekta binafsi huku ikivutia wawekezaji wapya kutoka ndani na nje ya Afrika.

Hatua hiyo imekuja wakati Soko la Hisa la Rwanda (RSE) na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji (CMA) zikikamilisha maandalizi ya mfumo wa kuruhusu bidhaa za kifedha zinazozingatia Sharia, ikiwemo sukuk, mifuko ya uwekezaji ya Kiislamu na REITs.

Kwa mujibu wa gazeti la The New Times, wadau wa sekta ya fedha wanaamini bidhaa hizo zitapanua vyanzo vya mtaji wa muda mrefu na kuwavutia wawekezaji ambao kwa sasa hawashiriki katika masoko ya kawaida kutokana na misingi yao ya kidini au maadili.

Mtendaji Mkuu wa RSE, Pierre Celestin Rwabukumba, alisema bidhaa hizo zitatoa fursa kwa kampuni zinazotafuta mtaji unaokidhi masharti ya Sharia pamoja na wawekezaji wanaotaka njia mbadala za uwekezaji.

Aliongeza kuwa mfumo huo utasaidia kuvutia mitaji kutoka Afrika Mashariki na nchi za Ghuba (GCC) huku ukipanua wigo wa bidhaa za uwekezaji zinazopatikana katika soko hilo.

Kwa mujibu wa The Citizen, Rwanda imekuwa nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki, Kati na Kusini kuweka kanuni maalumu za usajili na biashara ya bidhaa za masoko ya mitaji ya Kiislamu.

Kanuni hizo ziliandaliwa na kampuni ya Kitanzania ya Mayzuh Company Limited kwa ufadhili wa Luxembourg Aid and Development. Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Sheikh Mohamed Issa, ambaye amewahi pia kushiriki kuandaa mwongozo wa sukuk kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Tanzania (CMSA) mwaka 2022 pamoja na kuishauri Uganda kuhusu masoko ya mitaji ya Kiislamu, alisema mfumo huo umeweka mahitaji ya kisheria, kiudhibiti na ya uzingatiaji wa Sharia kwa bidhaa za masoko ya mitaji ya Kiislamu. Mkurugenzi Mkuu wa CMA Rwanda, Romeo Ngarambe, alisema kanuni zilizo wazi ni muhimu katika kuendeleza bidhaa zinazozingatia Sharia na kuimarisha miundombinu ya soko la mitaji nchini humo. Wadau wanaamini hatua hiyo inaweza kusaidia Rwanda kunufaika na soko la kimataifa la fedha za Kiislamu na kuimarisha nafasi yake kama kitovu cha ubunifu wa kifedha barani Afrika.

# Ukuaji wa benki za Kiislamu Afrika unahitaji nidhamu, si haraka

**NA UKHTI FATIMA SS**

**Katika ulimwengu wa biashara, mara nyingi mafanikio hupimwa kwa kasi ya ukuaji. Kampuni inapoongeza matawi mengi kwa muda mfupi, kuingia katika masoko mapya au kuongeza idadi ya wateja kwa haraka, hatua hizo huonekana kama ishara ya mafanikio.**

**Lakini katika sekta ya fedha za Kiislamu, wataalamu wengi wanaamini kuwa ukuaji wa haraka si lazima uwe ukuaji mzuri.**

**Mtazamo huo umejitokeza tena katika mjadala kuhusu mustakabali wa benki za Kiislamu barani Afrika. Wakati mahitaji ya huduma za kifedha zinazofuata misingi ya Shariah yakiendelea kuongezeka, viongozi wa sekta hiyo wanaonya kuwa upanuzi wa huduma hizo unapaswa kwenda sambamba na utawala bora, utaalamu na mifumo madhubuti ya usimamizi.**

**Benki za Kiislamu mara nyingi huchukuliwa kama huduma zinazolenga Waislamu pekee. Hata hivyo, wataalamu wa sekta hiyo wanaeleza kuwa msingi wake mkubwa si dini pekee bali ni maadili ya uwazi, uwajibikaji na kuhusisha shughuli za kifedha na uchumi halisi.**

**Tofauti na baadhi ya mifumo ya kifedha inayojikita katika biashara za madeni na miamala ya kubahatisha, fedha za Kiislamu zinataka shughuli za kifedha ziunganishwe na mali au shughuli halisi za kiuchumi. Hali hiyo imeifanya sekta hii kuvutia watu wanaotafuta uwazi na uaminifu katika huduma za kifedha, hata kama si Waislamu.**

**Afrika inaonekana kuwa na fursa kubwa katika eneo hili. Bara hili lina idadi kubwa ya watu ambao bado hawajafikiwa kikamilifu na huduma rasmi za kifedha. Wakati huo huo, ongezeko la matumizi ya teknolojia ya kidijitali limefungua milango mipya ya kufikisha huduma za kifedha kwa gharama nafuu.**

**Lakini wataalamu wanaonya kuwa fursa hiyo inaweza kupotea ikiwa taasisi zitakimbilia ukuaji bila kujenga mifumo imara ya usimamizi.**

**Moja ya changamoto kubwa katika fedha za Kiislamu ni suala la uaminifu. Mteja anayechagua benki ya Kiislamu anatarajia kuwa bidhaa anayopewa kweli inafuata misingi ya Shariah. Hivyo, taasisi husika zinapaswa kuwa na mifumo madhubuti ya usimamizi, bodi za ushauri wa Shariah, wataalamu wenye ujuzi na taratibu za kuhakikisha kuwa bidhaa zinazotolewa zinaendana na ahadi zinazotolewa kwa wateja.**

**Kwa maneno mengine, ukuaji wa benki za Kiislamu haupaswi kupimwa kwa idadi ya matawi pekee. Unapaswa kupimwa pia kwa uwezo wa taasisi husika kulinda uaminifu wa wateja.**

**Hoja hii ni muhimu hasa kwa Afrika ambako mazingira ya kisheria na udhibiti wa sekta ya fedha hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Mfumo unaofanya kazi vizuri katika nchi moja unaweza kuhitaji marekebisho makubwa kabla ya kutumika katika nchi nyingine.**




NA ABDULLAH RIFAT

# Je, vipi benki zingehifadhi akiba kwa thamani ya dhahabu?

Karibu kila benki ya kisasa duniani imejengwa juu ya msingi mmoja: riba. Watu huweka akiba zao benki, benki hukopesha fedha hizo kwa kiwango cha juu zaidi cha riba, na tofauti kati ya riba inayolipwa kwa wawekaji akiba na inayotozwa kwa wakopaji ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya benki.

Kwa watu wengi, huu ndiyo mfumo wa kawaida wa benki. Lakini kwa takribani Waislamu bilioni 1.8 duniani, suala la riba si rahisi kiasi hicho.

Sheria za Kiislamu zinakataza riba (riba), yaani faida ya uhakika inayotokana na mkopo. Marufuku hii inatokana na dhana kwamba fedha hazipaswi kuzalisha fedha zenyewe bila kushiriki hatari au shughuli halisi ya kiuchumi. Badala yake, faida na hasara zinapaswa kugawanywa kati ya pande zinazohusika.

Kwa miaka mingi, sekta ya fedha za Kiislamu imeunda njia mbalimbali mbadala za riba, ikiwemo mifumo ya kugawana faida, ukodishaji wa mali na mikataba ya mauzo yenye faida inayojulikana. Hata hivyo, baadhi ya wakosoaji bado wanaona kuwa baadhi ya bidhaa hizo zinafanana sana na mikopo ya kawaida ya riba, tofauti ikiwa ni muundo wa kisheria tu.




Kutokana na hali hiyo, wataalamu wengine wa fedha za Kiislamu wanaendelea kutafuta mifumo mbadala inayoweza kutofautiana zaidi na benki za kawaida.

Mojawapo ya mawazo yanayojadiliwa ni matumizi ya akaunti za akiba zinazoungwa mkono na dhahabu.

Katika mfumo huu, benki isingehifadhi akiba za mteja katika fedha za kawaida pekee. Badala yake, fedha za mteja zingebadilishwa kuwa thamani inayolingana ya dhahabu na benki ingeihifadhi kwa niaba yake.

Mteja anapotaka kutoa fedha zake, angepokea thamani ya dhahabu hiyo kwa bei ya soko ya wakati huo. Hivyo, hakuna riba inayolipwa wala mapato ya uhakika yanayotolewa.

Benki, kwa upande wake, isingepata mapato kupitia riba ya kukopesha fedha za mteja. Badala yake, ingeweza kutoza ada za uhifadhi, usimamizi au huduma nyingine zinazotolewa kwa uwazi.

Wafuasi wa wazo hili wanaona kuwa dhahabu ina sifa kadhaa zinazoiwezesha kutumika kama chombo cha kuhifadhi thamani kwa muda mrefu. Kwa karne nyingi, dhahabu imeendelea kutambuliwa kama mali yenye thamani na imeweza kustahimili vipindi vya mfumuko wa bei, misukosuko ya kisiasa na kushuka kwa thamani ya sarafu mbalimbali.

Katika historia ya Kiislamu, dhahabu na fedha zilikuwa msingi wa mifumo mingi ya fedha. Baadhi ya wanazuoni wanaamini kuwa marufuku ya riba ilikusudia kuzuia fedha zisitumiwe kama bidhaa ya kuzalisha faida zenyewe, bali kama njia ya kubadilishana thamani.

Mbali na hoja za kidini, wazo hili pia linavutia kwa sababu za kiuchumi. Tofauti na sarafu za kawaida ambazo zinaweza kupoteza thamani kutokana na mfumuko wa bei au sera za serikali, dhahabu imekuwa ikitazamwa kama mali yenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi thamani kwa muda mrefu.

Hata hivyo, mfumo huu una changamoto zake.

Kwanza, kuhifadhi dhahabu kwa kiwango kikubwa kunahitaji gharama kubwa za usalama na usimamizi. Pili, ingawa dhahabu huonekana kuwa imara kwa muda mrefu, bei zake zinaweza kupanda au kushuka kwa kiasi kikubwa katika muda mfupi. Hali hiyo inaweza kuwa changamoto kwa watu wanaohitaji fedha zao haraka.

Pia kuna changamoto za kisheria na kiudhibiti. Mifumo mingi ya benki duniani imejengwa juu ya matumizi ya sarafu za kawaida zinazotolewa na serikali. Kuanzisha akaunti zinazotegemea dhahabu kungehitaji mabadiliko makubwa ya sheria na mifumo ya usimamizi.

Aidha, wanazuoni wa Kiislamu wangepaswa kuchunguza kwa kina mfumo huo ili kuhakikisha kuwa unazingatia kikamilifu misingi ya Shariah.

Pamoja na changamoto hizo, waandishi na wataalamu wanaounga mkono mjadala huu wanaamini kuwa wazo hilo linastahili kujadiliwa kwa sababu linatoa nafasi ya kutafakari upya dhana ambazo watu wengi huzichukulia kuwa za kawaida. Swali muhimu si kama mfumo huu unaweza kutekelezwa mara moja, bali kama benki zinaweza kuendeshwa kwa namna tofauti na mfumo wa riba ambao umezoeleka kwa muda mrefu.

Kwa mtazamo huo, akaunti za akiba zinazoungwa mkono na dhahabu zinawakilisha jaribio la kutafuta mfumo wa kifedha unaolenga zaidi kuhifadhi thamani ya mali za watu kuliko kuzitumia kuzalisha mapato kupitia riba.

Makala imetafsiriwa na kufupishwa kutoka m

***akala ya Abdullah Rifat iliyochapishwa katika tovuti ya Prothomalo (https://en.prothomalo.com/amp/story/opinion/op-ed/eflt0c9uof)***

NA UKHTI FATIMA



# Kampuni zinavyopata mtaji wa kuendesha na kukuza biashara

**Biashara yoyote, iwe ndogo au kubwa, huhitaji mtaji ili kuanzishwa, kuendeshwa na kukua. Kampuni zinahitaji fedha za kununua mashine, kuongeza uzalishaji, kuajiri wafanyakazi, kuingia katika masoko mapya au kuanzisha bidhaa mpya.**
**Swali ambalo watu wengi hujiuliza ni: Kampuni hupata wapi fedha za kufanikisha mipango hiyo?**
**Kwa ujumla, kampuni hupata mtaji kutoka katika vyanzo viwili vikuu: vyanzo vya ndani ya kampuni na vyanzo vya nje ya kampuni.**

## Kutumia fedha za ndani ya kampuni

Njia ya kwanza ni kutumia fedha zinazozalishwa na biashara yenyewe. Hizi ni fedha ambazo kampuni huzipata bila kutegemea wakopeshaji au wawekezaji wa nje.

Mojawapo ya njia hizo ni kutumia sehemu ya faida iliyopatikana kutokana na shughuli za biashara. Badala ya kugawa faida yote kwa wamiliki au wanahisa, kampuni inaweza kubakiza sehemu yake na kuitumia kufadhili miradi mipya au kupanua shughuli zake.

Njia hii ina faida nyingi kwa sababu kampuni haiingii madeni wala kupunguza umiliki wa wamiliki waliopo. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachopatikana hutegemea kiwango cha faida ambacho biashara imezalisha.

Njia nyingine ni kuuza mali zisizotumika vizuri. Kampuni inaweza kuuza magari ya zamani, mashine zilizopitwa na wakati au majengo yasiyotumika na kutumia fedha hizo katika shughuli zenye tija zaidi. Pia kampuni inaweza kuongeza fedha kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Kupunguza gharama na kuongeza ufanisi wa matumizi kunaweza kuachia fedha za ziada kwa ajili ya uwekezaji.

## Ufadhili kutoka taasisi za kifedha

Wakati mwingine fedha za ndani hazitoshi kufanikisha mipango mikubwa ya biashara. Katika mazingira hayo, kampuni hutafuta mtaji kutoka taasisi za kifedha. Katika mfumo wa kawaida wa kifedha, kampuni nyingi hupata fedha kupitia mikopo yenye riba. Hata hivyo, katika mfumo wa fedha wa Kiislamu kuna njia mbadala zinazozingatia misingi ya Sharia.

Miongoni mwa njia hizo ni Murabaha, ambapo taasisi ya kifedha hununua bidhaa au vifaa vinavyohitajika na kampuni kisha kuviuza kwa bei inayojumuisha faida iliyokubaliwa. Pia kuna Musharaka, ambao ni mfumo wa ubia ambapo pande mbili au zaidi huchangia mtaji na kugawana faida na hasara kwa uwiano uliokubaliwa.

Njia nyingine ni Mudaraba, ambapo upande mmoja hutoa mtaji na upande mwingine hutoa utaalamu wa biashara. Faida hugawanywa kwa makubaliano ya awali huku hasara ya kifedha ikibebwa na mtoaji wa mtaji isipokuwa pale ambapo kuna uzembe au ukiukwaji wa makubaliano.

Mifumo hii inalenga kuwezesha biashara kupata mtaji bila kuhusika katika miamala ya riba ambayo imekatazwa katika Uislamu.

## Sukuk: mbadala wa hati fungani

Makampuni makubwa yanapohitaji fedha nyingi kwa ajili ya miradi mikubwa, yanaweza kutumia Sukuk.

Sukuk ni nyenzo ya uwekezaji inayofuata misingi ya Sharia. Tofauti na hati fungani za kawaida ambazo kwa kiasi kikubwa hujengwa juu ya deni lenye riba, Sukuk huwakilisha umiliki au ushiriki katika mali, huduma au mradi halisi wa kiuchumi.

Wawekezaji wanaonunua Sukuk hupata mapato yanayotokana na utendaji wa mali au mradi husika badala ya kupokea riba iliyowekwa mapema.

Katika miaka ya karibuni, Sukuk zimekuwa chanzo muhimu cha mtaji katika nchi nyingi duniani, zikiwemo nchi zisizo za Kiislamu. Hata Tanzania imeanza kushuhudia matumizi ya nyenzo hii kupitia taasisi mbalimbali za kifedha.

## Kuuza sehemu ya umiliki wa kampuni

Njia nyingine ya kupata mtaji ni kuuza sehemu ya umiliki wa kampuni kwa wawekezaji. Katika mfumo huu, unaojulikana kama 'equity financing', kampuni huuza hisa kwa wawekezaji na kupata fedha za kuendeleza biashara yake. Wawekezaji hao huwa sehemu ya wamiliki wa kampuni na hushiriki katika mafanikio yake kupitia gawio au ongezeko la thamani ya hisa.

Faida kubwa ya mfumo huu ni kwamba kampuni hailazimiki kurejesha fedha kama ilivyo kwenye mkopo. Hata hivyo, wamiliki wa awali hulazimika kugawana umiliki na mamlaka ya kufanya maamuzi na wawekezaji wapya.

## Kuingia katika soko la hisa

Baadhi ya kampuni huchagua kupata mtaji kwa kuuza hisa kwa umma kupitia soko la hisa. Hatua ya kwanza ya kuuza hisa kwa wananchi kwa mara ya kwanza huitwa Initial Public Offering (IPO). Kupitia mfumo huu, kampuni inaweza kukusanya kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwa wawekezaji wengi kwa wakati mmoja.

Baadaye kampuni inaweza kufanya mauzo mengine ya hisa ili kupata mtaji zaidi kadri mahitaji yanavyoongezeka. Njia hii imewezesha kampuni nyingi duniani kupanua shughuli zao na kuharakisha ukuaji wa biashara zao.

## Wawekezaji binafsi na ubia wa kimkakati

Kampuni changa au zinazokua kwa kasi mara nyingi hupata mtaji kutoka kwa wawekezaji binafsi. Wawekezaji hawa huweka fedha zao katika biashara kwa matarajio ya kupata sehemu ya faida ya baadaye. Mbali na mtaji, mara nyingi huleta utaalamu wa usimamizi, uzoefu wa biashara na mitandao ya masoko ambayo inaweza kusaidia kampuni kukua haraka zaidi.

ذو الحجة

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Waislamu tuwe mfano bora wa kutunza mazingira

Ijumaa iliyopita, Juni 5, 2026, Tanzania iliungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, tukio muhimu lililoasisiwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1972 kwa lengo la kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira.

Maadhimisho hayo yamefanyika duniani kote wakati huu ambapo kumekuwa na ongezeko la joto, ukame, mafuriko na majanga mengine katika mataifa mbalimbali yanayotokana na uharibifu wa mazingira.

Kutokana na unyeti wa kadhia hii ya uharibifu wa mazingira, kila mwanadamu amewajibishwa kuhakikisha anatunza na kulinda mazingira ili yanufaishe kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Kumbe basi, kutunza mazingira si suala la kijamii pekee bali ni ibada na sehemu ya utekelezaji wa mafundisho ya dini. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kuimarishwa kwake…" [Qur'an, 7:56].

Msingi wa aya hii unatokana na ukweli kwamba mazingira ndiyo nguzo ya maisha ya viumbe wote duniani. Binadamu, wanyama na mimea hutegemea mazingira kwa ajili ya mahitaji yao muhimu kama hewa safi, maji, chakula na makazi.

Kwa minajili hiyo, sisi Waislamu tunapaswa kuwa mstari wa mbele katika kushiriki shughuli za uhifadhi wa mazingira, ikiwamo kupanda miti, kutupa taka katika maeneo sahihi na kuepuka vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira.

Miongoni mwa vitendo hivyo ni matumizi ya nishati chafu ya kupikia, ukataji holela wa miti, uharibifu wa vyanzo vya maji, ufugaji wa kuhamahama na shughuli za viwandani zisizozingatia kanuni za uhifadhi wa mazingira.

Tukifanya hivyo, tutakuwa tumeweka msingi imara wa maisha bora na kuifanya dunia kuwa mahali salama kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine.

## Msimamo wa Uislamu kuhusu utunzaji wa mazingira

Uislamu, ambao ni mfumo kamili wa maisha ya binadamu, umeweka sharia na kanuni zinazowakinga watu dhidi ya madhara ya uchafuzi wa mazingira.

Sharia na kanuni hizo haziishii kwa mtu binafsi, familia na mazingira yanayomzunguka pekee, bali zinahusu ulimwengu mzima unaojumuisha mbingu, ardhi na vilivyomo ndani yake.

Qur'an tukufu imebainisha misingi ya kijiolojia (sayansi inayohusu umbo la dunia) na kutoa muongozo wa jinsi ya kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa mazingira.

Laiti watu wangefanyia kazi misingi hiyo, tatizo la mabadiliko ya tabianchi, ambalo kwa kiasi kikubwa linachochewa na shughuli za binadamu, lisingefikia kiwango kinachoshuhudiwa leo duniani. Cha kushangaza ni kwamba binadamu ndiyo wamekuwa vinara wa kuharibu mazingira.

Wanasahau kuwa mazingira wanayoishi nayo yanahitaji kutunzwa, kulindwa na kupendwa. Tunachokusudia kusema hapa ni kwamba kila kilichoumbwa na Mwenyezi Mungu kina lengo lake ambalo halina budi kutimizwa.

Anasema Mwenyezi Mungu: "Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliyomo baina yake ila kwa haki na kwa muda maalumu. Na waliokufuru wanayapuuza yale wanayoonywa." [Qur'an, 46:3].

Mwenyezi Mungu ameweka idadi kubwa ya rasilimali zinazolingana na mahitaji ya jumla ya wanadamu. Hii inaonesha kuwapo kwa uwiano wa rasilimali katika mazingira ya wanadamu.

Mwenyezi Mungu anasema: "Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo." [Qur'an, 54:49]. Aya hii inatoa taarifa ya jumla kuhusu uwepo wa uwiano katika kila kitu.

Na hakika si vinginevyo, mchakato wa uumbaji na ukuaji wa vitu vyote hufuata kanuni hii kama anavyoeleza Mwenyezi Mungu: "Na ardhi tumeitandaza, na tukaweka humo milima iliyosimama, na tumeotesha humo kila kitu kwa kiasi (kipimo) chake. Na tumekujaalieni humo vitu vya maisha yenu, na hao ambao nyinyi si wenye kuwaruzuku." [Qur'an, 15:19–20].

Tunachojifunza kutokana na aya hii ni kwamba vitu vyote vimeumbwa kwa ajili ya ustawi wa binadamu na viumbe wengine kulingana na ugavi aliouweka Mwenyezi Mungu. Hakuna shaka kuhusu wajibu wa binadamu katika kulinda na kuhifadhi mazingira.

ذو الحجة

KALAMU HURU

SEHEMU YA 1

SHEIKH Shaaban Mussa
0786 272 323

# Nini baada ya Hijja?

## Ni mwanzo wa mabadiliko siyo mwisho wa safari

**Msimu wa Hijja unapokaribia kuhitimishwa, mamilioni ya mahujaji huanza kurejea katika nchi zao wakiwa wamekamilisha nguzo ya tano ya Uislamu. Nyoyo zao hujaa furaha, macho yao hubeba kumbukumbu za maeneo matukufu, na ndimi zao huendelea kutaja Talbiyah walizozoea katika siku za Hijja.**

**Hata hivyo, pamoja na furaha hiyo, kuna swali muhimu ambalo kila hujjaji na kila Muislamu anapaswa kujiuliza: Nini baada ya hijja?**

**Swali hili ndilo msingi wa mfululizo huu wa makala zetu. Kwa sababu lengo la hijja halikuwa kufika Makka pekee, wala kutekeleza ibada kwa siku chache kisha maisha yarudi kama yalivyokuwa kabla yake. Hijja imekusudiwa kuwa shule ya mabadiliko ya maisha, madrasa ya kujenga ucha-Mungu na chuo cha kumuandaa Muislamu kwa safari ya utiifu wa Mwenyezi Mungu katika maisha yake yote.**

### Hijja ni zaidi ya safari

Watu wengi hujiandaa kwa miezi na miaka mingi kabla ya Hijja. Wengine huuza mali, wengine huweka akiba kwa muda mrefu, na wengine husubiri nafasi hiyo kwa hamu kubwa. Lakini mafanikio ya Hijja hayapimwi kwa ugumu wa safari wala gharama zilizotumika. Mafanikio yake hupimwa kwa athari zake katika moyo na maisha ya mhusika.

Ndiyo maana Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwenye kuhiji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, asiwe na maneno machafu wala kufanya maasi, atarejea kama siku aliyozaliwa na mama yake."

Hadith hii inadhihirisha kuwa Hijja ni fursa ya kusafishwa dhambi na kufungua ukurasa mpya wa maisha. Lakini mtu aliyefutiwa makosa yake anatakiwa aanze maisha gani baada ya hapo? Je, arejee katika mazoea yale yale aliyoyaacha kabla ya Hijja? Au aanze safari mpya ya utiifu na uongofu?

### Alama za Hijja Iliyokubaliwa

Wanazuoni wameeleza kuwa miongoni mwa alama za Hijja Mabrur ni kuonekana kwa mabadiliko ya kweli katika maisha ya mhusika. Hujaji anaporudi akiwa karibu zaidi na swala, mwenye mapenzi zaidi kwa Qur'an, mwenye huruma kwa watu na mwenye kujitenga na maasi, basi hayo ni katika dalili za kukubaliwa kwa Hijja yake.

Kinyume chake, ikiwa Hijja itabaki kuwa kumbukumbu ya picha, majina na simulizi za safari bila kuleta mabadiliko ya kitabia, basi mtu anapaswa kujitathmini upya. Kwa sababu ibada kubwa kama Hijja imekusudiwa kubadilisha maisha, si kuongeza hadhi ya kijamii pekee.

### Hijja na ujenzi wa taqwa

Mwenyezi Mungu ameifanya Taqwa kuwa lengo kuu la ibada nyingi. Katika Hijja, Muislamu hujifunza kujizuia na mambo ambayo kwa kawaida yanakuwa halali kwake. Hufundishwa uvumilivu, nidhamu na utiifu.

Anajifunza kwamba mja wa kweli ni yule anayetekeleza amri ya Mola wake Mlezi hata kama hajui hikima zote zilizomo ndani yake. Hivyo, baada ya Hijja anatakiwa kuendeleza roho hiyo ya utiifu katika maisha yake ya kila siku.

Ikiwa aliweza kuvumilia joto kali, msongamano mkubwa na uchovu kwa ajili ya kumtii Mwenyezi Mungu, basi anapaswa kuwa tayari kuvumilia changamoto za maisha kwa ajili ya kulinda dini yake na maadili yake.

### Kutoka Makka hadi nyumbani

Changamoto halisi ya Hijja huanza baada ya kurejea nyumbani. Ndani ya Ardhi Takatifu mazingira yote humsaidia mtu kufanya ibada. Lakini anaporudi katika mazingira yake ya kawaida hukutana tena na vishawishi, shughuli za dunia na majaribu ya kila siku.

Hapo ndipo inapodhihirika ikiwa Hijja ilikuwa tukio la muda mfupi au ilikuwa mwanzo wa mabadiliko ya kudumu. Muislamu mwenye kufaidika na Hijja hubeba roho ya Makka moyoni mwake hata baada ya kuondoka Makka.

Anabeba unyenyekevu alioujifunza, machozi aliyoyatoa katika dua, na ahadi alizomwekea Mola wake Mlezi. Hivyo maisha yake yote huwa mwendelezo wa yale aliyojifunza katika siku za Hijja.

### Hitimisho

Kwa hakika, Hijja si mwisho wa safari bali ni mwanzo wake. Ni mwanzo wa ukurasa mpya wa maisha, mwanzo wa uhusiano imara zaidi na Mwenyezi Mungu, na mwanzo wa juhudi mpya za kujenga nafsi na jamii.

Mafanikio ya Hijja hayapo katika siku zilizopita pekee, bali katika siku zinazofuata baada ya kurejea nyumbani. Hapo ndipo matunda ya Hijja huonekana na thamani yake hudhihirika.

Lakini kabla ya hujjaji kufika Arafah, Muzdalifah au Mina, kuna hatua moja muhimu sana ambayo ndiyo mlango wa kuingia katika ibada yote ya Hijja. Hatua hiyo ni kuingia katika Ihram. Kwa nini Uislamu umeweka umuhimu mkubwa kwa vazi hili maalumu? Ni mafunzo gani ya kiroho, kijamii na kimaadili yaliyofichwa ndani yake?

Hilo ndilo tutakalolichambua katika sehemu ijayo ya mfululizo huu: (Tumejifunza Nini Kutoka Katika Ihram?)

*Itaendelea...*

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Tufanye mabadiliko haya mashindano ya Qur'an

**Kwa miongo kadhaa sasa, Tanzania imeendelea kushuhudia ukuaji mkubwa wa mashindano ya Qur'an katika ngazi mbalimbali. Kutoka misikitini, madrasa, wilaya, mikoa hadi mashindano ya kitaifa na yale yenye hadhi ya kimataifa, juhudi hizi zimekuwa sehemu muhimu ya kukuza uhusiano wa Waislamu na Kitabu Kitukufu cha Allah Mtukuka.**

**Ni jambo la kujivunia kuona watoto, vijana na hata watu wazima wakijitokeza kwa wingi kushiriki mashindano hayo.**

**Wengi wamefanikiwa kuhifadhi sehemu kubwa za Qur'an huku wengine wakikamilisha kuhifadhi Qur'an yote. Haya ni mafanikio makubwa ambayo yanastahili kupongezwa.**

**Hata hivyo, wakati mafanikio haya yakiendelea kushuhudiwa, kuna haja ya kufanya tathmini ya kina kuhusu namna mashindano haya yanavyoendeshwa ili yaweze kuleta matokeo makubwa zaidi katika kujenga kizazi kinachoifahamu, kuielewa na kuishi kwa mujibu wa Qur'an.**

## Isiwe Ramadhan pekee

Kwa miaka mingi, imezoeleka kwamba mashindano mengi ya Qur'an huandaliwa zaidi katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Hakuna ubishi kwamba Ramadhan ni mwezi wa Qur'an. Ndani yake ndipo Qur'an ilipoteremshwa na ndani yake ibada nyingi huongezeka.

Lakini swali muhimu la kujiuliza ni hili: Je, Qur'an ni mwongozo wa mwezi mmoja tu katika mwaka?Jibu ni hapana.

Allah Aliyetukuka anasema katika Quran: "Hakika Qur'an hii inaongoza kwenye njia iliyo nyooka zaidi..." [Qur'an, 17: 9].

Aya hii haikuwekewa mipaka ya mwezi fulani. Qur'an ni mwongozo wa maisha yote, wa kila siku, kila mwezi na kila mwaka. Mafunzo yake yanagusa ibada, maadili, familia, uchumi, uongozi, elimu na uhusiano wa kijamii.

Kutokana na ukweli huo, mashindano ya Qur'an yanapaswa kuwa shughuli endelevu mwaka mzima.

Mashindano haya yasiwe matukio yanayosubiriwa Ramadhan pekee. Kila robo mwaka, kila nusu mwaka au kwa ratiba maalumu, mashindano yanaweza kuandaliwa ili kuwapa washiriki fursa ya kuendelea kujifunza na kujiendeleza.

Hatua hiyo itasaidia kuifanya Qur'an kuwa sehemu ya maisha ya kila siku badala ya kuhusishwa zaidi na msimu maalumu wa ibada.

## Tuongeze vionjo

Mabadiliko mengine muhimu yanayohitajika ni kupanua mawanda ya mashindano ya Qur'an.

Kwa sasa, sehemu kubwa ya mashindano mengi imejikita katika hifdh, yaani kuhifadhi aya za Qur'an kwa usahihi.

Bila shaka hifdh ni jambo adhimu lenye malipo makubwa mbele ya Allah Mtukuka. Waislamu wana kila sababu ya kuendelea kuhamasisha na kuunga mkono juhudi hizo.

Lakini pamoja na umuhimu wake, hifdh peke yake haitoshi.

Inawezekana mtu akahifadhi Qur'an yote lakini akawa na ufahamu mdogo kuhusu maana za aya, sababu za kushuka kwake, sheria zinazomo ndani yake au mafunzo makubwa yanayotokana nazo. Ndiyo maana kuna haja ya mashindano kuingiza vipengele vingine vya elimu ya Qur'an. Washiriki wanaweza kuulizwa maswali kuhusu tafsiri za aya mbalimbali, historia ya kushuka kwa sura, sababu za kuteremka kwa baadhi ya aya, pamoja na maudhui makuu yanayopatikana katika sura tofauti za Qur'an.

Vilevile washindani wanaweza kupimwa katika elimu za tajwid, qiraat, ulumul Qur'an na hata namna Qur'an inavyozungumzia masuala ya kijamii, kisayansi, kimazingira na kimaadili.

Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunajenga kizazi kisichohifadhi tu maneno ya Qur'an bali pia kinachoyafahamu na kuyatumia katika maisha ya kila siku.

## Kuandaa wataalamu wa Qur'an

Tanzania inahitaji zaidi ya wahifadhi wa Qur'an. Inahitaji pia wataalamu wa Qur'an.

Nchi inahitaji vijana wanaoweza kueleza kwa ufasaha ujumbe wa Qur'an kwa jamii ya leo. Inahitaji wanaoweza kujibu maswali yanayohusu Qur'an katika nyanja mbalimbali za maisha. Inahitaji watafiti, walimu, wanazuoni na wahubiri wenye uelewa mpana wa sayansi nzima ya Qur'an.

Mashindano yanaweza kuwa daraja muhimu la kufikia lengo hilo. Badala ya kutazama ushindani kama tukio la kupata washindi na zawadi pekee, yawe sehemu ya mchakato wa kutengeneza viongozi wa kielimu wa kesho. Mfumo wa maswali unaweza kuhamasisha washiriki kusoma vitabu vya tafsiri, kujifunza historia ya Qur'an na kufanya utafiti wa kina kuhusu mafunzo yake.

Matokeo yake yatakuwa ni kupata kizazi chenye uwezo wa kuwasilisha ujumbe wa Qur'an na kuifanya Qur'an kuwa sehemu ya maisha ya kila siku badala ya kuhusishwa zaidi na msimu maalumu wa ibada.

ذو الحجة

فتاوى



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

# Upi ubora wa mwezi wa Muharram?

**Swali: Ni upi ubora wa mwezi wa Muharram?**

**Jibu:** Mwenyezi Mungu amesema: "Hakika idadi ya miezi mbele ya Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na miwili katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu tangu alipoziumba mbingu na ardhi. Miongoni mwake ipo miezi minne mitakatifu. Huo ndiyo mfumo ulio sawa wa dini. Basi msijidhulumu nafsi zenu ndani ya miezi hiyo." [Quran, 9: 36].

Na katika Hadith sahihi zilizopokewa na Bukhari na Muslim, kutoka kwa Abu Bakrah (Allah amridhie), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwaka una miezi kumi na miwili; miongoni mwake ipo miezi minne mitakatifu: mitatu inafuatana, nayo ni Dhul-Qa'dah, Dhul-Hijjah na Muharram; na Rajab wa Mudhwar ulio kati ya Jumada na Shaaban."

Miezi hii imeitwa mitakatifu (hurum) kwa sababu ya utukufu wake mkubwa na nafasi yake mbele ya Mwenyezi Mungu. Katika miezi hii thawabu huzidishwa, dhambi huwa kubwa zaidi kwa uzito wake, na watu hukatazwa kufanya dhuluma na uadui.

Na katika Sahih Muslim, kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Funga iliyo bora zaidi baada ya Ramadhan ni katika mwezi wa Mwenyezi Mungu, Muharram. Na swala iliyo bora zaidi baada ya swala za faradhi ni swala ya usiku."

Kwa hiyo, mwezi wa Muharram una ubora wake kwa mambo mawili: Kwanza, Ni miongoni mwa miezi mitakatifu ambayo Mwenyezi Mungu ameipa heshima na utukufu mkubwa. Pili, imependekezwa kukithirisha saumu za sunna ndani yake, hasa siku ya Ashura na siku ya Tasu'a.

Kufunga siku ya Ashura ni kafara ya dhambi ndogo za mwaka mmoja uliopita, ilhali kufunga siku ya Tasu'a ni miongoni mwa sifa maalumu za umma huu wa Kiislamu.

Hata hivyo, haikupendekezwa kuufunga mwezi wote wa Muharram, kwa sababu katika hadith sahihi iliyopokewa na Bukhari na Muslim kutoka kwa Ibn Abbas (Allah amridhie), amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (Allah amshushie rehema na amani) hakuwahi kufunga mwezi mzima kabisa isipokuwa Ramadhan."

Kwa hiyo, Sunna ni kufunga sana katika Muharram, hasa Tasu'a na Ashura, lakini si kuufunga mwezi wote mzima. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

**Swali: "Ni ipi hukumu ya kufunga ndoa katika mwezi wa Muharram?"**

**Jibu:** Ni kwamba wapo baadhi ya watu wa kawaida huamini kuwa kufunga ndoa katika mwezi wa Muharram ni jambo linalochukiza (makruhu) kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.

Hata hivyo, imani hii haina msingi wowote katika dini ya Kiislamu, bali ni miongoni mwa dhana potofu za watu. Kwa msingi huo, inajuzu (inaruhusiwa) kufunga ndoa katika mwezi wa Muharram kama ilivyo katika miezi mingine yote. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

**Swali: Kuna mwanagu ameniambia kuna ndoto anaiota inajirudia rudia ikionesha. Katika ndoto hiyo, anamuona mdogo wake tuliyemzika miezi kadhaa nyuma anakuja mlangoni anagonda akisema "Dada nifungulie nina njaa sijala muda mrefu." Na kila akiota anaota hivyo hivyo,. Sasa je hii tafsiri yake ni nini?**

**Jibu:** Kuhusu ndoto kama hii, haifai kutoa tafsiri ya moja kwa moja kwa uhakika, kwa sababu tafsiri za ndoto zinahitaji elimu, mazingira ya muotaji, na mara nyingi ndoto hazibebi maana ya hakika. Kwa ujumla, wanazuoni wameeleza kuwa kumuona marehemu katika ndoto akilalamika njaa au haja fulani kunaweza kuwa na maana kadhaa, miongoni mwao:

Mosi, huenda ni mawazo na huzuni za aliyebaki hai, hasa ikiwa kifo ni cha karibuni na mdogo wake alikuwa akimpenda sana. Akili inaweza kuendelea kurejesha kumbukumbu zake katika ndoto.

Pili, inaweza kuwa ni ukumbusho wa kumwombea marehemu, kumtakia Maghfirah, na kutoa sadaka kwa niaba yake, ikiwa inawezekana. Marehemu hunufaika na dua za walio hai.

Tatu, si lazima iwe ishara kwamba marehemu ana njaa halisi au anateseka. Mambo ya ulimwengu wa Barzakh hatuyajui isipokuwa kwa yale yaliyothibiti katika Qur'an na Sunna.

NASAHA ZA WIKI 0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Makosa haya katika sala yanaharibu ibada yako

Allah Mtukufu ameifanya sala kuwa miongoni mwa ibada za msingi zinazomlazimu Muislamu kuzitekeleza kila siku, kwa kuwa ndiyo ibada ya kwanza ambayo mja atahesabiwa kwayo Siku ya Kiyama.

Ni kwa sababu hiyo, Waislamu wamehimizwa kuitekeleza kwa usahihi, unyenyekevu na kwa kufuata mafundisho ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Pamoja na ukweli huo, bado baadhi ya Waislamu hujikuta wakifanya makosa mbalimbali katika sala; mengine yakitokana na ukosefu wa elimu na mengine kutokana na mazoea yaliyojengeka kwa muda mrefu.

Miongoni mwa makosa yanayoonekana mara kwa mara ni kuingia msikitini kwa kukimbia ili kuipata rakaa inayokaribia kuisha. Ingawa nia yao huwa njema, mafundisho ya dini yanasisitiza kuielekea sala kwa utulivu na heshima.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametwambia: "Mnaposikia iqama, ziendeeni sala kwa utulivu na uchamungu, wala msikimbie. Rakaa mtakazoziwahi swalini, na mtakazozikosa zikamilisheni." [Bukhari na Muslim].

Kumtangulia Imam au kwenda sambamba naye

Baadhi ya maamuma hurukuu au kusujudu kabla ya Imam, jambo ambalo limekatazwa katika Uislamu.

Katika misikiti mingi, hasa wakati wa sala za jamaa, baadhi ya watu humtangulia Imam katika rukuu, sijida au kunyanyuka kutoka katika nguzo mbalimbali za sala. Wengine huenda sambamba naye kana kwamba wanashindana naye.

Jambo hili linapingana na mafundisho ya Mtume, ambayo yanamtaka maamuma wamfuate Imam katika kila hatua ya sala. Mtume amesema: "Hakika Imam amewekwa ili afuatwe." [Ahmad na Abu Daudi].

## Kutotulizana katika rukuu na sijida

Hili ni kosa jingine linaloonekana kwa baadhi ya waswaliji. Wapo wanaorukuu kwa sekunde chache tu kabla ya kunyanyuka, huku wengine wakisujudu kwa haraka sana bila kuipa sijida haki yake.

Pia wapo wanaonyanyuka kutoka rukuu na kwenda moja kwa moja katika sijida bila kusimama kwa utulivu. Wanazuoni wameeleza kuwa utulivu katika nguzo za sala ni sehemu muhimu ya ukamilifu wa ibada hiyo.

## Kukosa khushuu (utulivu)

Ukosefu wa khushuu ni tatizo kubwa linalowakumba Waislamu wengi. Mtu husimama mbele ya Mola wake kwa ajili ya sala, lakini mawazo yake yanakuwa katika biashara, familia au mipango mbalimbali ya maisha.

Matokeo yake mwili unakuwa katika sala huku moyo ukiwa mbali na ibada hiyo.

## Kutokusoma vizuri Suratul–Fatiha

Tatizo jingine ni kutokusoma Suratul–Fatiha kwa usahihi. Baadhi ya Waislamu huisoma sura hiyo kwa haraka mno au kwa matamshi yasiyo sahihi, huku wakipuuza kujifunza kusoma Qur'an kwa usahihi. Makosa ya matamshi na usomaji wa haraka huathiri ubora wa sala na yanaweza kupunguza utimilifu wake.

## Kutonyoosha safu

Katika sala za jamaa, baadhi ya Waislamu huacha nafasi kubwa kati yao na wenzao, huku wengine wakisimama mbele au nyuma ya safu bila sababu au udhuru unaokubalika kisharia.

Pia wapo wasiyoziba mianya katika safu za sala. Badala ya kusogea kwenye nafasi zilizo wazi, hubaki waliposimama, jambo linalosababisha safu kuwa na mapengo yasiyo ya lazima.

Hali hiyo huondoa uzuri na nidhamu inayotakiwa katika ibada ya pamoja. Mtume amesema: "Nyoosheni safu zenu, kwani kunyooka kwa safu ni katika ukamilifu wa sala." [Bukhari na Muslim].

Aidha, baadhi ya Waislamu huchezea nguo, saa, kofia au ndevu zao wanapokuwa katika sala. Vitendo hivyo huwanyima umakini na wakati mwingine huwasumbua wanaosali karibu nao.

Kosa jingine ni kugeuza macho huku na kule badala ya kuyaelekeza mahali pa kusujudia. Wengine huwatazama watu wanaoingia msikitini au kufuatilia kila kinachoendelea pembeni yao.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amekataza kugeuza macho wakati wa sala na akasisitiza umuhimu wa kuzingatia ibada kwa moyo na viungo vyote.

Miongoni mwa makosa mengine ni kutotuliza viungo saba vya sijida ipasavyo, ambavyo ni paji la uso na pua, viganja viwili vya mikono, magoti na vidole vyote vya miguu.

Kwa ujumla, makosa hayo huathiri khushuu, hupunguza malipo ya sala na wakati mwingine yanaweza kubatilisha sala ikiwa yanahusiana na nguzo au masharti muhimu ya sala. Aidha, huondoa utukufu na uzito wa sala, ambayo ni mawasiliano ya moja kwa moja kati ya mja na Mola wake.

Wanazuoni wameeleza kuwa ukamilifu wa sala unategemea mambo makuu matatu. Kwanza kuitekeleza kwa kuzingatia wakati wake maalumu; pili kuitekeleza dhahiri yake vizuri kwa maneno na vitendo; na tatu kuitekeleza kwa moyo wenye unyenyekevu na khushuu.

Maana ya kuitekeleza sala kikamilifu ni kuhudhurisha moyo ndani yake. Hicho ndicho kiini cha kusimamisha sala kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

Tatizo kubwa linalochangia makosa mengi katika sala ni ukosefu wa elimu. Waislamu wengi hujifunza kusali kwa kuwaangalia wazazi wao au watu waliowazunguka bila kutafuta elimu ya kina kuhusu hukumu na taratibu za sala.

Elimu ndiyo njia bora ya kurekebisha makosa hayo. Hivyo, ni wajibu wa kila Muislamu kujifunza fiqhi ya sala ili aweze kuitekeleza ibada hiyo kwa usahihi, unyenyekevu na kwa kufuata mafundisho ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

ذُو الحِجَّة

MAKALA MAALUM

SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811



# Hukumu na fadhila za kumzuru mgonjwa

Kumzuru mgonjwa ni katika adabu tukufu ambazo Uislamu umehimiza Waislamu kuzizingatia, na umeifanya kuwa miongoni mwa haki muhimu za Muislamu juu ya ndugu yake Muislamu.

Pia ni miongoni mwa njia za kuleta upendo baina ya nyoyo za waumini. Allah Mtukufu anasema: "Na shikamaneni na kamba ya Allah nyote pamoja, wala msifarakane." [Qur'an, 3:103].

Kumzuru mgonjwa humfanya ajihisi kuwa ndugu zake Waislamu wanamjali na kumthamini katika kipindi cha maradhi yake. Hali hiyo huchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza maumivu na huzuni anazopitia.

Aidha, humpa faraja na kumsaidia kurejesha matumaini, sambamba na kumfidia baadhi ya yale aliyoyakosa wakati alipokuwa na afya na nguvu.

Miongoni mwa adabu za wema waliotangulia ni kwamba walipokuwa hawajamuona mwenzao walikuwa wakimuulizia. Akiwa safarini walimwombea dua na kuiangalia familia yake; akiwa nyumbani walimtembelea, na akiwa mgonjwa walimzuru.

Baadhi ya wanazuoni wanaona kuwa kumzuru mgonjwa ni faradhi kifaya, ambayo ikifanywa na baadhi ya watu hutosheleza kwa wengine. Hoja yao inatokana na kauli ya Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) aliposema: "Walisheni wenye njaa, watembeleeni wagonjwa, na muwakomboe mateka." [Bukhari].

Wanazuoni wamejengea hoja hadith hii kwamba kumtembelea mgonjwa kunamhusu kila mgonjwa; awe mwanaume au mwanamke, mkubwa au mdogo, Muislamu au asiye Muislamu, bila kujali aina ya ugonjwa wake.

Jopo la Wanazuoni (Jumhur) wamesema kuwa kumtembelea mgonjwa ni jambo linalopendeza (Sunna) – iwe mgonjwa huyo unamfahamu au humfahamu, awe ndugu au mtu wa mbali.

Hitimisho lenye nguvu (rajihi) ni kwamba kumtembelea mgonjwa kunaweza kuwa wajibu kwa baadhi ya watu kama ndugu, jamaa na majirani, na kuwa sunna kwa wengine.

Ni vema mtu akachagua muda unaofaa wa kumtembelea mgonjwa, wala asimtembelee wakati ambao unamletea uzito.



## Sunna za kumzuru mgonjwa

Ni sunna kumfariji mgonjwa na kumkumbusha hekima ya Allah kwamba ugonjwa unafuta madhambi. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alikuwa akisema pindi anapowazuru wagonjwa: "Laa ba'sa twahuur Insha Allah." Yaani hakuna ubaya, ugonjwa unafuta madhambi.

Aidha, Mtume amesema: "Haumpati Muislamu uchovu, wala maradhi, wala msongo, wala huzuni, wala maumivu, wala dhiki, hata mwiba unaomchoma, isipokuwa Allah humfutia kupitia hayo makosa yake." [Bukhari na Muslim].

Pia ni sunna kumuuliza mgonjwa hali yake na kumfariji. Ikiwa hawezi kuzungumza, basi unaweza kuwauliza wale anaoishi nao kuhusu hali yake.

Ni wajibu kwa anayemzuru mgonjwa kumkumbusha matokeo mazuri ya subira, kumhimiza kuridhia, na kumsomea aya na hadith zinazotuliza moyo wake na kuondoa huzuni yake. Vilevile, amjulishe kuwa Allah anawapenda wenye subira na kwamba malipo makubwa huambatana na ukubwa wa mtihani.

Ni muhimu pia kumkumbusha mgonjwa kwamba kulalamika na kulaani ugonjwa hakuondoi ugonjwa, bali humfanya apoteze malipo na huenda akapata madhambi.

Vilevile, amkataze mgonjwa kutamani kifo na aihimize familia yake kuwa na subira katika kumhudumia na kumtendea wema. Mara nyingi, watu wa karibu wa mgonjwa huchoka au humwona mgonjwa kama mzigo, hususan pale ugonjwa unapodumu kwa muda mrefu au kuwa katika hali mbaya, hali inayoweza kuwafanya wapunguze juhudi za kumhudumia.

## Dua ya kumuombea mgonjwa

Aidha, imesuniwa kwa anayemzuru mgonjwa kumwombea dua na kumfanyia ruqya (dua za tiba).

Imepokewa hadith kutoka kwa mama Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake) akieleza kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akisema pindi anapomzuru mgonjwa: "Ewe Mola wa watu! Ondosha maradhi, mpe shifaa, kwani wewe ndiye Mponyaji. Hakuna uponyaji ila uponyaji wako, uponyaji usiyoacha ugonjwa wowote." [Bukhari na Muslim].

Pia kumsomea dua hii: "Kwa jina la Allah, nakusomea ruqya kutokana na kila kinachokuumiza, kutokana na shari ya kila nafsi au jicho la mwenye husuda. Allah akuponye..."

Pia dua isemayo: "Najilinda kwa maneno kamili ya Allah dhidi ya kila shetani, kila kiumbe chenye sumu, na kila jicho baya." Kisomo cha ruqya kinaruhusiwa mradi kisiwe na ushirikina ndani yake.

Inaruhusiwa kumtafutia mgonjwa daktari wa kumtibu, na ikiwezekana mgonjwa mwanaume atibiwe na daktari mwanaume, na mwanamke atibiwe na daktari mwanamke. Lakini ikiwa kuna dharura, inaruhusiwa kinyume chake.

Kadhalika, ni sunna kutoa sadaka kwa ajili ya kuomba uponyaji. Mtume amesema: "Watibuni wagonjwa wenu kwa sadaka." [Abu Daud, Bayhaqi na wengineo].

Aidha, ni sunna kumtamkisha shahada anapokaribia kufa. Mtume amesema: "Wafundisheni waliokaribia kufa kusema: 'Laa ilaaha illa Allah.'" Maneno haya husemeshwa mgonjwa mwenye fahamu na anayeweza kuzungumza. Akishatamka shahada, usiirudie tena ili asichoke au kukerwa.

## Usizidishe muda wa ziara

Baadhi ya watu hukaa muda mrefu kwa mgonjwa, jambo ambalo linapingana na mwongozo wa Uislamu katika kumzuru mgonjwa na katika ziara kwa ujumla.

Miongoni mwa adabu muhimu za kumzuru mgonjwa ni kumpa matumaini ya kupona kwa idhini ya Allah, na kutomuumiza kwa kumkumbusha waliokufa kutokana na ugonjwa huo. Mtume amesema: "Mnapomtembelea mgonjwa mpeni matumaini ya kuishi, kwani hilo halizuii chochote (katika makadirio ya Allah) bali humfariji mgonjwa."

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383




# Uongozi bora huanza na kusikiliza watu

Miaka kadhaa iliyopita, mfanyabiashara mmoja aliyefanikiwa aliulizwa siri ya mafanikio yake katika kujenga mtandao mkubwa wa marafiki, wateja na washirika wa biashara. Wengi walitarajia atazungumzia elimu yake, akili yake au mbinu zake za biashara.

## Badala yake alitoa jibu lililowashangaza wengi.

"Nimejifunza kusikiliza," alisema.

Alieleza kuwa watu wengi huingia kwenye mazungumzo wakitaka kusikika, kushinda hoja au kutoa ushauri. Wachache huingia wakitaka kuelewa. Kadiri miaka ilivyopita, aligundua kuwa uwezo wa kusikiliza ulikuwa umemfungulia milango mingi kuliko uwezo wake wa kuzungumza.

Katika dunia ya leo iliyojaa simu za mkononi, mitandao ya kijamii na ratiba zenye shughuli nyingi, kusikiliza kwa makini kumekuwa nadra. Watu wengi husikia maneno, lakini hawasikilizi kwa dhati. Ndiyo maana wataalamu wa mawasiliano wanasema kusikiliza ni moja ya stadi muhimu zaidi katika mahusiano, kazi na maisha kwa ujumla.

## Huunda mazingira salama ya mazungumzo

Wasikilizaji wazuri hujenga mazingira ambayo watu wanajisikia salama kuzungumza.

Mtu anapohisi kwamba hatatahukumiwa, hatachekwa wala kukataliwa kwa sababu ya mawazo yake, huwa tayari zaidi kueleza hisia na changamoto zake kwa uwazi.

Kinyume chake, mtu anayekatiza mazungumzo kila mara, anayebeza maoni ya wengine au anayekimbilia kulaumu huwafanya watu wajifiche na kutosema yaliyo moyoni mwao.

Katika familia, mazingira ya aina hii huwasaidia wanandoa na watoto kuwasiliana kwa uhuru. Kazini, huongeza ushirikiano na kuimarisha mahusiano kati ya wafanyakazi.

## Hutambua hisia za wengine

Moja ya sifa za wasikilizaji wazuri ni uwezo wao wa kuthamini hisia za watu wengine. Badala ya kusema, "Unafanya jambo hili kuwa kubwa kuliko lilivyo," husema, "Ninaelewa kwa nini jambo hili limekuumiza."

Kauli kama hizi hazimaanishi kwamba wanakubaliana na kila kitu kinachosemwa. Badala yake, zinaonyesha kwamba wametambua hisia za mtu mwingine. Mara nyingi watu hawahitaji suluhisho la haraka. Wanahitaji kwanza kuhisi kuwa wameeleweka. Hilo peke yake linaweza kupunguza migogoro mingi katika mahusiano.

## Huongozwa na udadisi wa kujifunza

Wasikilizaji wazuri wana tabia ya kuuliza maswali kwa lengo la kuelewa zaidi.Badala ya kudhani tayari wanajua kila kitu, huwa na udadisi wa kujifunza kutoka kwa wengine. Huuliza maswali yanayofungua mazungumzo badala ya kuyafunga.

Tabia hii huwasaidia kupata maarifa mapya, kuelewa mitazamo tofauti na kujenga uhusiano wa karibu zaidi na watu wanaowazunguka.

Kwa hakika, watu wengi hupenda kuzungumza na mtu anayewauliza maswali ya dhati kuliko anayejizungumzia muda wote.

Hutoa umakini kamili

Katika zama za teknolojia, watu wengi hujaribu kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja. Mtu anaweza kuwa anazungumza na wewe huku akiangalia simu, televisheni au kompyuta. Tatizo ni kwamba mawasiliano ya kweli huhitaji umakini.

Wasikilizaji wazuri huweka pembeni vitu vinavyoweza kuwavuruga na kuelekeza fikra zao kwa mtu anayezungumza. Lugha ya mwili wao huonyesha kwamba wako pamoja na mzungumzaji.

Kitendo hicho rahisi huwasilisha ujumbe wenye nguvu: "Ninakuheshimu na ninachokisema kina thamani kwangu."

## Husikia zaidi ya maneno

Wakati mwingine ujumbe muhimu hauko katika maneno yanayotamkwa bali katika namna yanavyosemwa. Mtu anaweza kusema, "Niko sawa," lakini sauti yake, uso wake au mwenendo wake ukaonyesha kwamba kuna tatizo.

Wasikilizaji wazuri huangalia ishara hizi. Wanasikiliza sauti, huzingatia hisia na kutambua lugha ya mwili. Hii huwasaidia kuelewa ujumbe wa kina ambao huenda haujasemwa moja kwa moja.

Ndiyo maana mara nyingi huwa watu wa kwanza kugundua kwamba rafiki, mwenza au mwanafamilia anapitia changamoto fulani.

Uislamu unahimiza kusikiliza kwa hekima

Mafundisho ya Kiislamu yanasisitiza umuhimu wa kusikiliza kabla ya kuzungumza. Mwenyezi Mungu amewasifu wale wanaosikiliza maneno na kufuata yaliyo bora miongoni mwake.

Kusikiliza kwa makini ni ishara ya unyenyekevu, heshima na busara. Kunamwezesha mtu kuelewa kabla ya kuhukumu na kujibu kabla ya kugombana.

Watu wengi hutumia miaka mingi kujifunza kuzungumza vizuri, lakini wachache hutumia muda kujifunza kusikiliza vizuri. Hata hivyo, uwezo wa kusikiliza unaweza kuboresha ndoa, kuimarisha urafiki, kuongeza mafanikio kazini na kujenga jamii yenye maelewano zaidi.

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

# Je, AI inalea kizazi cha wavivu kufikiri?



Katika miaka michache iliyopita, akili bandia (AI) imeingia kwa kasi katika maisha yetu. Leo mwanafunzi anaweza kuandika insha, kutatua hesabu, kutafsiri lugha au kupata muhtasari wa kitabu kwa sekunde chache kupitia programu kama ChatGPT na nyingine zinazofanana nayo.

Kwa wazazi na walimu wengi, maendeleo haya yanaonekana kuwa habari njema. Mtoto anapata msaada wa haraka na kazi zinafanyika kwa urahisi zaidi. Lakini baadhi ya wataalamu wa elimu na saikolojia wanaanza kuuliza swali muhimu: Je, urahisi huu unasaidia watoto kuwa werevu zaidi au unawafanya wawe wavivu kufikiri?

Swali hili si la kupuuzwa.

Tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa watu wanapotumia AI kupata majibu ya moja kwa moja, kiwango cha ushiriki wa ubongo katika kutatua tatizo hupungua. Kwa lugha rahisi, mashine inafanya sehemu ya kazi ambayo hapo awali ilifanywa na akili ya binadamu.

Kwa mtu mzima, athari zake zinaweza kuwa ndogo kwa sababu tayari amejenga misingi ya kufikiri, kuchambua na kutatua matatizo. Lakini kwa mtoto ambaye bado anajenga uwezo huo, hali inaweza kuwa tofauti.

Fikiria mtoto anayejifunza kuendesha baiskeli. Ikiwa kila wakati mtu mwingine atasukuma baiskeli badala yake, atafika mbali zaidi kwa muda mfupi. Lakini hatajifunza kuendesha baiskeli mwenyewe.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa kufikiri.

Mtoto anayepata majibu kutoka kwa AI kabla hajajaribu kufikiri mwenyewe anaweza kumaliza kazi ya shule haraka. Lakini swali ni je, ubongo wake umejifunza nini katika mchakato huo?

Wataalamu wa maendeleo ya watoto wanaeleza kuwa ubongo hukua kupitia changamoto. Kila mtoto anapokutana na tatizo, anapochanganyikiwa kidogo, anapojaribu njia tofauti na hatimaye kupata suluhisho, njia mpya za neva hujengwa katika ubongo wake.

Kwa maneno mengine, ugumu si adui wa kujifunza. Ugumu ni sehemu ya kujifunza.

Tatizo ni kwamba AI imeundwa kuondoa ugumu huo. Hiyo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Inatoa majibu ya haraka, maelezo mafupi na suluhisho zinazookoa muda. Lakini kile kinachookoa muda kinaweza pia kuondoa fursa ya ukuaji wa akili.

Hii haimaanishi kuwa AI ni mbaya. Kama ilivyo kwa teknolojia nyingi, manufaa au madhara yake hutegemea jinsi inavyotumiwa. Mtoto anaweza kutumia AI kama mwalimu wa ziada anayetoa maelezo baada ya yeye kujaribu mwenyewe. Anaweza kutumia kuuliza maswali ya nyongeza au kupata mifano zaidi ya kuelewa somo.

Tatizo linaanza pale AI inapochukua nafasi ya kufikiri kwa mtoto.

Kwa mfano, badala ya kuandika insha yake mwenyewe na kuomba AI ipendekeze maboresho, mtoto anaweza kuiomba AI iimwandikie insha yote. Badala ya kujaribu kutatua hesabu, anaweza kuipiga picha na kusubiri jibu.

Katika hali hiyo, mtoto amepata matokeo lakini hajapata ujuzi.

Wazazi wana jukumu muhimu katika kipindi hiki. Badala ya kuuliza tu kama kazi imekamilika, wanaweza kuuliza maswali kama: “Uliifikiriaje?” “Ulikwama wapi?” au “Ni jambo gani jipya umejifunza?”

Maswali hayo humsaidia mtoto kuthamini mchakato wa kujifunza badala ya jibu la mwisho pekee. Walimu pia wanaweza kuwahimiza wanafunzi kueleza walivyofikia majibu yao badala ya kuwasilisha majibu pekee.

Ukweli ni kwamba dunia ya kesho itakuwa na AI yenye uwezo mkubwa zaidi kuliko ya leo. Hivyo, thamani ya binadamu haitapimwa kwa uwezo wa kupata taarifa haraka. Itapimwa kwa uwezo wa kufikiri kwa kina, kuhoji, kuhukumu na kufanya maamuzi sahihi.

Hayo ni mambo ambayo hakuna mashine inayoweza kufanya kwa niaba ya mtoto. Kwa hiyo, changamoto si kuwazuia watoto kutumia AI. Changamoto ni kuhakikisha kuwa AI inakuwa chombo cha kuwasaidia kufikiri zaidi, si sababu ya wao kufikiri kidogo.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 11



# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

**Ndugu msomaji, utakumbuka kwamba mwanzoni mwa makala yetu tulieleza kuwa hakuna habari iliyoelezwa kwa upana zaidi katika Qur'an kuliko habari za nabii Musa na kizazi cha Israil. Na jina "Musa" ndilo lililotajwa mara nyingi zaidi katika Qur'an kuliko majina yote. Kwa hali hiyo, katika mwendelezo wa makala yetu tutajitahidi kufanya udondozi katika kila eneo linalowahusu angalau kwa muhtasari. Lengo ni kujenga uelewa wa kutosha juu ya kaumu (kizazi) hiki kwani kila nukta ya maisha yao ina ibra (mazingatio) makubwa.**

## Fir-aun afazaika

Baada ya wachawi kushindwa na kuuona ukweli kulikowapelekea kusilimu pale pale uwanjani, Fir-aun pamoja na wakuu wenzake walibabaika na wakahamaki kweli kweli.

Malengo ya Mfalme Fir-aun; kumshinda Musa na kuwazuia watu kumuamini Mola wake kupitia wachawi, lilifeli. Kisha, wachawi hao wakawa wa kwanza kuukubali ukweli.

Kwa kipindi kirefu, Fir-aun alidhani kuwa amezimiliki nyoyo za watu kama alivyovimiliki viwiliviwili vyao. Alijidanganya kuwa amezitawala akili za watu wote wa Misri kama alivyozitawala na kuzinyamazisha sauti zao, na kwamba, katika nchi yake hakutakuwa na yoyote atakayeamini kinyume na anachokiamini yeye au bila ya rukhsa yake.

Naam, kwani ndiye huyu huyu aliyekuwa akiwaambia raia zake: ...mimi`sikupeni shauri ila niliyoiona (kuwa nzuri) na sikuongozeni ila kwenye njia ya uongofu." [Qur'an, 40:29]. Hii ndiyo sababu Fir-aun alifazaika sana pale mambo yalipomuendea kombo na kuwa kinyume na alilolitarajia.

Fir-aun alin'gaka na kuwatisha wachawi: " Oh! Mnamuamini (Musa) kabla sijakuruhusuni? Bila shaka huyu ni mkubwa wenu aliyekufundisheni uchawi, basi mtajua (mtaona nitakachokufanyeni). Nitaikata mikono yenu na miguu yenu kwa kubadilishana (mkono wa kulia kwa mguu wa kushoto, na mguu wa kushoto kwa mkono wa kulia), na kisha nitakusulubuni nyote." [Qur'an, 26:49].

Katika aya ya 71 sura ya 20 imekuja: "....na nitakusulubuni katika mashina ya mitende, na hakika mtajua kati yetu (mimi na mungu wa Musa) nani aliye mkali wa kuadhibu na kuiendeleza (adhabu)."

## Majibu ya wachawi

"Wakasema, 'Haidhuru, hakika sisi tunarejea kwa Mola wetu. Bila shaka sisi tunatumai ya kwamba Mola wetu atatusamehe madhambi yetu kwani sisi tumekuwa wa kwanza wa wenye kusilimu (hapa)." [Qur'an, 26:50-51].

Tusome tena majibu hayo mahala pengine: "Tunaapa kwa yule Aliyetuumba, hatutakuhiari wewe tukaacha zile ishara zilizotufikia. Basi fanya unavyotaka kufanya, wewe unaweza kutoa hukumu ya maisha haya haya ya dunia. Kwa yakini sisi tumemuamini Mola wetu ili atusamehe makosa yetu na (kufanya) uchawi uliotulazimisha, na Mwenyezi Mungu ni Mbora na wa kudumu, (siyo wewe)." [Qur'an, 20:72-73].

Walizidi kuonesha msimamo wao wa kumkataa Fir-aun kwa kusema: "(Potelea mbali), sisi tumerudi kwa Mola wetu, nawe hukuona baya lolote kwetu ila kuwa tumeziamini aya (miujiza) ya Mola wetu ilipotufikia..." Kisha wakamuomba Mola wao wakasema..."Mola wetu, tumiminie subira na utufishe hali ya kuwa Waislamu." [Qur'an, 7:126].

Kwa kweli yalikuwa mapinduzi ya kweli ya Imani na ujasiri wa ajabu ambao ni nadira kutokea katika historia za mitume na kaumu zao. Mara tumeona watu maarufu katika jamii (Almalau) ndiyo wa kwanza kupinga da'wa ya Mitume.

## Viongozi wamtia mori Fir-an

Hasira za mkuu huyo zilipanda zaidi baada ya kuendewa na waheshimiwa mawaziri wake na kumuomba amchukulie hatua kali Musa na jamaa zake (Wana wa Israil).

Qur'an inasema: "Na wakuu katika watu wa Fir-aun (mawaziri na usalama wa taifa) walisema, 'Je utamuacha Musa na watu wake walete uharibifu katika nchi na kukuacha wewe na waungu wako (uliotaka waabudiwe pamoja na wewe)?"

Yaani wanataka kumwambia: "Hivi kweli serikali yako inashindwa kukishuhulikia kikundi kidogo cha wahuni chenye nia ya kuleta vurugu, uvunjifu wa amani na kutishia kuiangusha serikali yako?" Akasema: "Tutaendelea kuwaua watoto wao wa kiume na kuwaacha hai wanawake wao, na bila shaka sisi ni wenye nguvu juu ya hayo." [Qur'an, 7:127].

"Na akasema Fir-aun niacheni nimuue Musa naye amwite Mola wake. Mimi nachelea asije kuiharibu dini yenu au kuleta matata katika nchi." Musa akasema: "Mimi najikinga kwa Mola wangu na Mola wenu na kila mwenye jeuri asiyeamini siku ya hesabu." [Qur'an, 40:26-27].

ذوالحجة

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

# Mazingira machafu, afya hatarini

Mtu anaposikia habari za mabadiliko ya tabianchi, ukataji miti au uchafuzi wa mazingira, mara nyingi huona ni mada zinazohusu wanasayansi, wanamazingira au viongozi wa serikali. Lakini ukweli ni kwamba suala la mazingira ni suala la afya pia.

Hewa tunayovuta, maji tunayokunywa, chakula tunachokula na mazingira tunamoishi vina uhusiano wa moja kwa moja na afya zetu. Ndiyo maana wataalamu wa afya duniani wanaonya kwamba uharibifu wa mazingira umegeuka kuwa moja ya vitisho vikubwa vya afya ya binadamu katika karne ya 21.

Katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu, Umoja wa Mataifa na Shirika la Afya Duniani (WHO) wametoa onyo kwamba madhara ya mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira si tatizo la kesho, bali ni tatizo linaloua watu leo.

## Hewa chafu inaua kimya kimya

Miongoni mwa athari kubwa za mazingira kwa afya ni uchafuzi wa hewa.

Kulingana na WHO, mamilioni ya watu duniani hufariki kila mwaka kutokana na magonjwa yanayohusishwa na hewa chafu. Uchafuzi huo huongeza hatari ya magonjwa ya moyo, kiharusi, saratani ya mapafu na magonjwa mbalimbali ya mfumo wa upumuaji.

Katika baadhi ya miji mikubwa duniani, viwango vya uchafuzi wa hewa vimefikia kiwango kinachoweka mamilioni ya watu katika hatari ya kiafya kila siku. Hata watoto wadogo, wazee na watu wenye magonjwa sugu ndiyo wanaobeba mzigo mkubwa zaidi wa madhara hayo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres amesema dalili za janga la mazingira sasa zinaonekana wazi kupitia hewa iliyochafuliwa, ardhi iliyoharibiwa na mifumo ya ikolojia inayoporomoka. Athari hizo tayari zinadhuru afya za watu na kuhatarisha maisha yao.

## Joto kali linaongeza magonjwa na vifo

Miaka ya karibuni imekuwa miongoni mwa miaka yenye joto zaidi kuwahi kurekodiwa duniani.

Kadiri joto linavyoongezeka, ndivyo hatari za kiafya zinavyoongezeka pia. Mawimbi ya joto kali yanaweza kusababisha upungufu wa maji mwilini, matatizo ya moyo, uchovu mkali na hata vifo.

WHO imeonya kuwa ongezeko la mawimbi ya joto linaendelea kuongeza kiwango cha magonjwa na vifo katika maeneo mengi duniani. Watu wanaofanya kazi nje, wazee na wagonjwa huwa katika hatari kubwa zaidi. Mbali na madhara ya moja kwa moja, joto kali pia huathiri uzalishaji wa chakula na upatikanaji wa maji safi, hali inayoweza kusababisha matatizo mengine ya kiafya.

## Mafuriko na ukame huleta magonjwa

Mabadiliko ya tabianchi yameongeza matukio ya hali mbaya ya hewa kama mafuriko, ukame na dhoruba. Mafuriko yanaweza kuharibu miundombinu ya maji na usafi wa mazingira, jambo linaloongeza hatari ya magonjwa yanayoenezwa kupitia maji machafu kama kipindupindu na kuhara.

Kwa upande mwingine, ukame unaweza kusababisha uhaba wa maji salama na chakula. Hali hiyo huongeza utapiamlo, hasa kwa watoto, na kudhoofisha kinga ya mwili dhidi ya magonjwa.

WHO imeeleza kuwa majanga ya hali ya hewa pia huchochea kuenea kwa magonjwa yanayoenezwa na wadudu kama mbu, huku yakivuruga huduma za afya na ugavi wa dawa katika maeneo yaliyoathirika.

## Afya ya akili nayo inaathirika

Mara nyingi watu huzungumzia madhara ya mazingira kwa mwili pekee, lakini afya ya akili nayo huathirika.

Kupoteza makazi kutokana na mafuriko, kuharibika kwa mashamba kutokana na ukame au kupoteza chanzo cha kipato kutokana na uharibifu wa mazingira kunaweza kusababisha msongo wa mawazo, hofu na mfadhaiko.

WHO imeonya kuwa hatari kwa afya ya akili na ustawi wa kisaikolojia zinaongezeka kadiri athari za tabianchi zinavyozidi kuwa kubwa.

Kwa familia nyingi, majanga ya mazingira si habari za televisheni bali ni matukio yanayobadilisha maisha yao kabisa.

## Chakula na maji salama viko hatarini

Uharibifu wa mazingira pia unaathiri usalama wa chakula.

Ardhi inapoharibika, misitu kupotea na mifumo ya mvua kubadilika, uzalishaji wa mazao hupungua. Hali hiyo huongeza njaa na utapiamlo, hasa katika nchi zinazoendelea.

Nchini Nigeria, wataalamu wameonya kuwa uchafuzi wa mazingira, ukataji miti, uchimbaji holela wa madini na uchomaji gesi umechangia kuharibika kwa mashamba, kupungua kwa samaki na kuongezeka kwa magonjwa. Athari hizo zimezidisha umaskini, kupunguza uzalishaji na kuongeza gharama za afya.

## Kila mtu ana jukumu

Ingawa serikali na makampuni makubwa yana wajibu mkubwa wa kulinda mazingira, wananchi nao wana nafasi muhimu.

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

ذو الحجة

# Mtume alivyoishi na wakeze

**Kutoka kwa mama Aisha (Allah amuwie radhi) amesema: "Siku moja nilisafiri na Mtume (rehema na amani zimshukie) katika baadhi ya safari zake nikiwa bado msichana mdogo na mwembamba." Mtume akawaambia watu: "Tangulieni mbele." Kisha akaniambia: "Njoo tushindane mbio." Basi tukashindana, hatimaye nikampita.**
**Katika safari nyingine, nikiwa nimenenepa kidogo, aliwaambia watu: "Tangulieni." Kisha akaniambia: "Njoo tushindane tena." Nikashindana naye, hatimaye akanishinda.**
**Mwisho Mtume akacheka na kuniambia: "Hii nimelipiza ile ya mwanzo."" *[Abu Daudi]."***

## Mafundisho ya tukio

Mtume (rehema na amani zimshukie) ametuachia mfano bora na kielelezo cha juu katika kila jambo, ikiwamo namna ya kujenga familia yenye mafungamano imara na kuishi kwa wema ndani ya familia

Allah Mtukufu ametuusia kuishi vema na wake zetu aliposema: "Na kaeni nao kwa wema..." [Qur'an, 4:19].

Katika maisha yetu ya sasa, tunashuhudia madhila na matatizo makubwa wanayokumbana nayo wanawake kutokana na miamala mibaya ya waume zao, vipigo, manyanyaso na kukosa huduma muhimu za dharura katika maisha ya kila siku.

Kesi nyingi bado zinasubiri maamuzi ya kuvunja ndoa kutokana na ugumu wanaokutana nao katika maisha. Hali hii inakwenda kinyume na muongozo na mwenendo wa Mtume (rehema na amani zimshukie).

Mtume alipitia mazingira yote tunayohitaji. Alikuwa mume, baba na kiongozi katika jamii, hivyo ni wajibu kumtii na kumuiga. Aliyesoma sira (wasifu) ya Mtume (rehema na amani zimshukie) hashangazwi na uzuri wa tabia yake na namna alivyokuwa na uhusiano mwema na watu wa jamii zote.

Zaidi ya hayo, Mtume alionesha upendo na wema wa hali ya juu kwa watu wa nyumbani mwake, hususan wake zake, kwa namna ya kipekee. Allah amemsifu Mtume kwa kusema: "Na hakika wewe (Muhammad) uko juu ya tabia tukufu kabisa." [Qur'an, 68:4].

Kuhusu tabia ya Mtume kwa ujumla wake, mama Aisha (Allah amuwie radhi) alisema kwa kifupi: "Tabia ya Mtume ilikuwa ni Qur'an." [Muslim]. Tukio hili linaonesha namna Mtume alivyokuwa karibu na wakeze, akiwatania, akicheza nao na kufanya utani unaokubalika kisheria.

## Uvumilivu kwa wakeze

Kuna wakati Abubakr (Allah amridhie) alimtembelea Mtume, ghafla akamsikia mama Aisha akimsemesha Mtume kwa sauti ya juu. Abubakr aliingia ndani akiwa na hasira, akasema: "Ewe binti wa Umm Ruman! Unampazia sauti mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Mtume (rehema na amani zimshukie) akasimama kati yao kuwazuia. Baada ya Abubakr kutoka, Mtume alimwambia Aisha kwa upole: "Hivi huoni kuwa nimemzuia yule mtu (baba yako) asiwe mkali kwako?"

Abubakr alirejea baadaye na kumkuta Mtume na Aisha wanacheka, akasema kwa utani: "Ewe Mtume wa Allah, nishirikishe sasa katika amani yenu kama mlivyonishirikisha katika ugomvi wenu." [Abu Daudi na Ahmad].

Hadith hii inaonesha kuwa Mtume hakuwa mwepesi kunyanyua mkono wake kuwapiga wakeze hata pale walipomkosea. Maisha ya Mtume kwa wake zake ni kielelezo bora cha mapenzi, wema, upole, unyenyekevu na kusaidiana.

Amesema Mtume: "Mbora wenu ni yule aliye mbora kwa watu wa nyumbani mwake, nami ni mbora wenu kwa watu wa nyumbani mwangu." [Tirmidhi].

Naye mama Aisha (Allah amuwie radhi) amesema: "Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akihudumia watu wa nyumbani mwake (akiwasaidia kazi zao), na aliposikia wito wa swala alitoka kwenda kuswali." [Bukhari katika Adab al–Mufrad].

Mama Aisha anaendelea kusema: "Mtume wa Allah alikuwa akishona nguo zake mwenyewe, akitengeneza viatu vyake na kufanya kazi zote ambazo wanaume hufanya kwenye nyumba zao." [Ahmad].

## Upendo, huruma na heshima

Anas bin Malik (Allah amridhie) amesimulia kuwa alimuona Mtume (rehema na amani zimshukie) akikunja nguo yake ili Safiya (mkewe) apande juu yake. Kisha akaweka goti lake chini, Safiya akalikanyaga na kumpanda ngamia wake, [Bukhari].

Mtume alikuwa na huruma, mpole, mwadilifu, mcheshi, na aliwaheshimu sana wakeze. Pia alikuwa akishirikiana nao katika kazi za nyumbani. Hakuwa akilipa ubaya kwa ubaya, bali alikuwa msamehevu na mwenye kusema ukweli.

Kwa hiyo, Mtume alikuwa kielelezo bora cha namna ya kuishi kwa amani, upendo na maelewano kwa watu wa familia yake.

## Kuhudumia familia ni ibada, si udhaifu

Mtume alionesha kuwa mume anaposhiriki kazi za nyumbani hupata thawabu na kujenga mapenzi ya kweli. Ushirikiano baina ya watu wa familia huondoa migogoro na kuimarisha uhusiano mwema, upendo na umoja.

Thawabu na ujira mkubwa kwa Allah hupatikana katika mambo madogo madogo kama kushona nguo, kufua au kuosha vyombo. Sasa jiulize. Ikiwa Mtume alifanya kazi za nyumbani kwake, kwa nini wewe hufanyi?




MAKALA MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Usimtatulie kila tatizo, msaidie mtoto ajifunze kutatua

Mtoto wa miaka saba anajaribu kufunga kamba za viatu vyake. Anajaribu mara moja, mara mbili, mara tatu. Kamba zinakataa kutii. Baada ya dakika chache anasema kwa sauti ya kukata tamaa, "Mama, nisaidie."

Mama ana chaguo mbili. Anaweza kupiga magoti na kufunga kamba hizo ndani ya sekunde chache. Au anaweza kusema, "Jaribu tena. Niko hapa nikikuangalia."

Wazazi wengi huchagua njia ya kwanza. Ni ya haraka, ni rahisi na inaonekana kuwa ya upendo. Lakini wataalamu wa malezi wanaonya kwamba wakati mwingine msaada wa haraka sana humwibia mtoto fursa muhimu ya kujifunza.

Mzazi mmoja aliwahi kusimulia kwamba mwanawe alifikisha miaka 11 bila kujua kufunga kamba za viatu. Sababu haikuwa kwamba mtoto alikuwa na tatizo lolote. Tatizo lilikuwa kwamba kila mtu nyumbani alikuwa na haraka kila siku na hivyo walikuwa wakimfanyia kazi hiyo. Walipogundua hali hiyo, walitambua kuwa walichodhani ni msaada kilikuwa kimemnyima mtoto stadi muhimu ya kujitegemea.

## Watoto hujifunza kwa kufanya

Moja ya kanuni muhimu za malezi ni kwamba watoto hujifunza zaidi kwa kufanya kuliko kwa kuangalia.

Mtoto hawezi kujifunza kuandaa kitanda chake ikiwa kila siku mzazi ndiye anayekitandika. Hawezi kujifunza kuwajibika kwa vitu vyake ikiwa kila mara kuna mtu anayekimbia kuokoa hali baada ya kusahau.

Wakati mwingine wazazi huamini wanawasaidia watoto wao kwa kuwafanyia mambo mengi. Lakini ukweli ni kwamba watoto hujenga uwezo, kujiamini na ustahimilivu wanapopewa nafasi ya kufanya mambo wenyewe.

## Usitoe jibu kabla hajafikiri

Fikiria mtoto anayefanya kazi ya nyumbani ya shule na anakwama swali la hesabu.

Badala ya kumpa jibu moja kwa moja, mzazi anaweza kuuliza, "Umejaribu njia gani mpaka sasa?" au "Unafikiri unaweza kuanzia wapi?"

Maswali kama haya humfundisha mtoto kufikiri. Yanamwonyesha kwamba matatizo yanaweza kuchambuliwa na kutatuliwa hatua kwa hatua.

Kinyume chake, mtoto anayepata majibu tayari kila wakati hujifunza kutegemea wengine badala ya kuamini uwezo wake wa kufikiri.

## Kubali fujo na kutokamilika

Wazazi wengi hufanya kila kitu kwa niaba ya watoto kwa sababu hawawezi kuvumilia makosa, fujo au kuchelewa.

Ni rahisi zaidi kumvika mtoto nguo kuliko kusubiri dakika kumi akijaribu mwenyewe. Ni rahisi zaidi kuosha vyombo upesi kuliko kumruhusu mtoto avioshe na kuacha matone ya maji mezani.

Lakini kujifunza kunahitaji nafasi ya kufanya makosa.

Mtoto anayejifunza kupika atamwaga unga. Anayejifunza kufua anaweza kutumia sabuni nyingi. Anayejifunza kupanga chumba anaweza kufanya makosa kadhaa kabla hajafaulu.

Hayo si matatizo ya malezi. Hiyo ndiyo sehemu ya malezi.

## Kila tatizo si la mzazi

Watoto wawili wanagombania mpira. Wazazi wengi hukimbilia kuwa waamuzi wa haraka. Lakini wakati mwingine suluhisho bora ni kuwauliza watoto wenyewe waeleze kilichotokea na wapendekeze namna ya kumaliza mgogoro.

Kwa kufanya hivyo, wanajifunza kusikiliza, kujadiliana, kusamehe na kutafuta suluhisho. Hizi ni stadi muhimu ambazo watahitaji maisha yao yote.

Bila shaka, mzazi anapaswa kuingilia kati pale usalama au ustawi wa mtoto unapokuwa hatarini. Lakini si kila mgogoro mdogo unahitaji mzazi kuwa mwamuzi.

## Usiyogope mtoto kuchoka

Katika zama za simu za mkononi na televisheni, wazazi wengi huharakisha kuwapa watoto burudani wanaposema, "Ninachoka."

Lakini kuchoka si adhabu. Mara nyingi ndiyo chanzo cha ubunifu.

Mtoto anayechoka anaweza kuanza kusoma kitabu, kuchora, kutengeneza mchezo wake au kubuni hadithi mpya. Ubongo wake huanza kutafuta suluhisho badala ya kusubiri mtu mwingine amburudishe.

## Jiulize swali la kesho

Wataalamu wengi wa malezi hupendekeza wazazi kujiuliza swali moja muhimu: "Ikiwa siku moja sitakuwepo, mtoto wangu ataweza kufanya jambo hili mwenyewe?"

Ikiwa mtoto mkubwa hajui kufua nguo zake, kuandaa chakula rahisi, kusafisha chumba chake au kuwajibika kwa ratiba zake, huo ni ujumbe kwamba kuna stadi za maisha ambazo bado zinahitaji kufundishwa.

Lengo la malezi si kumfanya mtoto awe tegemezi milele. Lengo ni kumwandaa kwa maisha ya kujitegemea.

Wazazi wote wanapenda kuwaona watoto wao wakifanikiwa. Lakini mafanikio hayo hayajengwi kwa kuwaondolea kila changamoto. Yanajengwa kwa kuwafundisha namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Dalili tano zinazoonyesha umechoka kiakili na kihisia

Kila mtu huchoka. Baada ya siku ndefu ya kazi, safari au shughuli nyingi, ni kawaida kuhisi uchovu. Hata hivyo, kuna aina nyingine ya uchovu ambayo si rahisi kuiona. Huu ni uchovu wa akili na hisia.

Tofauti na uchovu wa mwili, ambao mara nyingi hupungua baada ya kupumzika au kulala, uchovu wa kiakili na kihisia unaweza kuendelea kwa muda mrefu bila mtu kutambua. Wakati mwingine hujificha nyuma ya hasira, kukosa motisha, kujitenga na watu au kupoteza hamu ya kufanya mambo ambayo zamani yalikuwa rahisi.

Wataalamu wa afya ya akili wanaeleza kuwa kutambua dalili mapema kunaweza kumsaidia mtu kuchukua hatua kabla hali haijawa mbaya zaidi.

## Kazi ndogo zinaonekana kuwa mzigo mkubwa

Moja ya dalili za kwanza za uchovu wa kiakili ni pale kazi ndogo zinapoanza kuonekana ngumu kupita kawaida.

Mambo ambayo hapo awali yalikuwa sehemu ya kawaida ya maisha yanaanza kuhisi kama mzigo mkubwa. Unaweza kujikuta unahisi kuchoshwa na ombi dogo kutoka kwa mwenzako, mtoto au mfanyakazi mwenzako.

Tatizo si ukubwa wa kazi yenyewe. Mara nyingi tatizo ni kwamba akili na hisia tayari zimeelemewa na mambo mengi kiasi kwamba hata jukumu dogo linaonekana kama mzigo mkubwa.

## Mabadiliko madogo yanakuvuruga sana

Maisha yana mabadiliko ya kila siku. Miadi inaweza kubadilika, ratiba inaweza kuchelewa au mpango uliowekwa unaweza kutofanyika kama ulivyotarajiwa.

Mtu mwenye utulivu wa kiakili mara nyingi huweza kuzoea mabadiliko hayo bila shida kubwa. Lakini mtu aliyefikia kiwango cha uchovu wa kihisia anaweza kujikuta akikasirika sana au kuvunjika moyo kwa sababu ya jambo dogo tu.

Hii hutokea kwa sababu uwezo wa akili wa kukabiliana na changamoto mpya huwa umepungua kutokana na uchovu uliokusanyika kwa muda mrefu.



## Hata majukumu ya kawaida yanahitaji nguvu nyingi

Dalili nyingine ni kuhisi kwamba lazima ujisukume sana ili kutekeleza majukumu ya kawaida.

Kuamka asubuhi, kwenda kazini, kujibu simu, kufanya usafi au kushiriki katika shughuli za familia kunaweza kuanza kuhisi kama kazi kubwa sana.

Wakati mwingine watu hujilaumu kwa hali hii wakidhani ni uvivu. Lakini mara nyingi tatizo si uvivu bali ni akiba ndogo ya nguvu za kiakili na kihisia zilizobaki ndani yao.

## Unaona wanaokuzunguka kama maadui

Uchovu wa kihisia unaweza kubadilisha namna mtu anavyowaona wengine.

Mtu anaweza kuanza kuhisi kwamba watu hawamwelewi, hawamjali au wanamwongezea matatizo badala ya kumsaidia. Hata ushauri wa kawaida unaweza kuonekana kama ukosoaji au mashambulizi binafsi.

Matokeo yake, mahusiano huanza kuharibika. Migogoro huongezeka na mtu hujikuta akijitenga na watu ambao kwa kawaida wangekuwa chanzo cha msaada na faraja.

Ndiyo maana wataalamu wa saikolojia husisitiza umuhimu wa kutambua hali hii mapema kabla haijaathiri familia, urafiki au mazingira ya kazi.

## Hata kujitunza kunaonekana kuchosha

Dalili nyingine inayopuuzwa mara nyingi ni kupoteza hamu ya kujitunza.

Mtu anaweza kuacha kufanya mazoezi, kula vizuri, kusoma vitabu, kutembelea marafiki au kushiriki katika shughuli zinazompa furaha. Wengine huanza kupunguza hata muda wa kupumzika kwa sababu kila kitu kinaonekana kuwa kinahitaji nguvu nyingi.

Tatizo ni kwamba kujitunza ndiko kunakoweza kusaidia kurejesha nguvu za akili na hisia. Hivyo mtu huingia katika mzunguko mbaya ambapo uchovu husababisha kuacha kujitunza, na kuacha kujitunza huongeza uchovu zaidi.

## Nini kifanyike?

Hatua ya kwanza ni kukubali kwamba umechoka. Watu wengi hujaribu kuendelea kuvumilia bila kikomo wakidhani hali itapita yenyewe.

Hatua nyingine ni kutafuta mapumziko ya kweli. Hii inaweza kujumuisha kupunguza ratiba zisizo za lazima, kulala vya kutosha, kufanya mazoezi, kuzungumza na watu unaowaamini au kutafuta ushauri wa kitaalamu pale inapohitajika.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, ibada pia ni sehemu muhimu ya kuimarisha afya ya akili. Swala, dua, kusoma Qur'an na kumtegemea Mwenyezi Mungu humsaidia Muumini kupata utulivu wa moyo katikati ya changamoto za maisha.

Uchovu wa kiakili na kihisia si udhaifu wala kushindwa. Ni ishara kwamba akili na moyo vinahitaji mapumziko, msaada au mabadiliko fulani katika maisha.

Kadiri unavyotambua dalili hizi mapema, ndivyo unavyoongeza nafasi ya kurejesha nguvu, utulivu na furaha kabla hali haijaathiri afya yako, kazi yako na mahusiano yako na watu wanaokuzunguka.